

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Hamsini na Nane – Tarehe 24 Juni, 2021

(Bunge Lilianza Saa Tatoo Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:

Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa Mwaka 2019/2020.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Katibu.

NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Maswali, tutaanza na Ofisi ya Rais TAMISEMI. Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Ndanda sasa aulize swalii lake.

Na. 485

Utoaji wa Namba Vijiji vya Jimbo la Ndanda

MHE. CECIL D. MWAMBE aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itasaidia na kufanikisha kutoa Namba kwa Vijiji vya Chipunda, Mkalinda na Sululu ya Leo vyenye wakazi zaidi ya elfu kumi katika Jimbo la Ndanda?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Jimbo la Ndanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Vijiji vya Chipunda na Sululu ni vijiji halali ambavyo vimeendelea pia kutambulika kuptitia Matangazo ya Serikali Namba 536 Mamlaka za Miji na 537 Mamlaka za Wilaya ya tarehe 19/07/2019. Vijiji hivyo pia vilishiriki kikamilifu katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika mwaka 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na changamoto ya uchakavu na upotevu wa Hati za Usajili za baadhi ya Vijiji, mwaka 2019/2020, Ofisi ya Rais – TAMISEMI ilihiusha taarifa za vijiji vyote nchini na kuandaa kanzidata ya Hati za Usajili wa

Vijiji vyote nchini kwa kuzingatia matakwa ya kifungu cha 22 na 26 cha Sheria ya Serikali za Mitaa, Mamlaka za Wilaya, Sura ya 287. Hati hizo kwa sasa zipo katika hatua ya uchapishaji na zitatolewa kwa vijiji vyote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na zoezi hilo, Kijiji cha Chipunda kilichopo Kata ya Mkululu, Halmashauri ya Wilaya ya Masasi Namba yake ya Usajili ni MTR-091-0900989. Kijiji cha Sululu kilichopo Kata ya Sululu, Halmashauri ya Mji wa Masasi Namba yake ya Usajili ni MTR-092-09011574. Kijiji cha Mkalinda hakipo katika Orodha ya Vijiji vilivyopo nchini.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Cecili Mwambe, swali la nyongeza.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Labda tu nitaarifu Meza yako kwamba kwa bahati mbaya sana sikupatiwa jibu la swali hili kabla ya sasa hivi, majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri yanatofautiana kabisa kwa sababu wamechanganya taarifa zilizopo Halmashauri ya Wilaya ya Masasi na zilizopo Halmashauri ya Wilaya ya Mji Masasi. Vijiji hivyo vinafanana lakini kimsingi majibu yaliyopatikana ni tofauti na ambavyo mimi nilivyopeleka swali langu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Cecil Mwambe, majina ya vijiji yanafanana?

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ndio, kwenye swali langu nilisema Sululu ya Leo lakini kwenye jibu anasema Sululu, Sululu iko Kata ya Sululu, Halmashauri ya Wilaya ya Masasi Mji, Sululu ya Leo iko Kata ya Namatutwe, Halmashauri ya Masasi *DC*.

NAIBU SPIKA: Kwa maelezo haya hili swali halijajibiwa. Hii Sululu ya Leo ina maana hili neno Leo ni sehemu ya jina ya hicho Kijiji. Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri itabidi hili swali lijibewe upya baada ya kupata taarifa hizo za kutoka Ndanda kwa Mheshimiwa Cecil David Mwambe.

Mheshimiwa Saashisha nilikuona lakini kwa sababu swali halijajibiwa haliwezi kuwa na swali la nyongeza. Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 486

Kuanzisha Wilaya Mpya ya Ukonga-Dar es Salaam

MHE. MARIAM N. KISANGI aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Wilaya mpya ya Ukonga katika Halmashauri ya Wilaya ya Ilala?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Mheshimiwa David Ernest Silinde, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la Ukonga liko katika Wilaya ya Ilala ambayo ni moja kati ya Wilaya tano zinazounda Mkoa wa Dar es Salaam. Utaratibu wa kuanzisha Mkoa na Wilaya mpya umebainishwa kuitia Sheria ya Uanzishwaji wa Mikoa na Wilaya Na. 397 ya mwaka 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kuanzisha Wilaya mpya huanzia kwenye Serikali za Vijiji/Mitaa ili kupata ridhaa ya wananchi kisha hupelekwa kwenye Mabaraza ya Madiwani ya Halmashauri, Kamati ya Ushauri ya Wilaya (*DCC*) na Kamati ya Ushauri ya Mkoa (*RCC*). Baada ya hatua hiyo, maombi hayo huwasilishwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa ajili ya uhakiki na kujiridhisha na baadaye kuwasilishwa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Ilala bado hajijawasilisha maombi hayo kadri ya matakwa ya sheria.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, swali la nyongeza.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa kuwa mchakato wa kuanzisha Wilaya ya Ukonga ulifanywa mwaka 2015 sambamba na uazishwaji wa Wilaya ya Kigamboni na Ubungo katika halmashauri mbili ambazo wakati huo Mkoa wa Dar es Salaam ulikuwa na Halmshauri ya Temeke, Ilala na Kinondoni. Kwa hiyo, Wilaya zote za Mkoa wa Dar es Salaam zillifanya mchakato wa kutaka kuongeza halmashauri ikiwemo Halmashauri ya Wilaya Ukonga. Je, Serikali haioni haja sasa ya kurudia kwenye kumbukumbu zake kuangalia jambo hilo ili lifanyiwe utaratibu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwanza, niipongeze Serikali kwa kuanzisha Jiji la Dar es Salaam lakini kwa kuwa Ofisi za Halmashauri ya Jiji ziko katika Mtaa wa Morogoro *Road na Drive Inkwa* kifupi mjini Posta na kwa mkazi wa Chanika, Msongora, Mzinga, Kitunda, Zingiziwa, wana changamoto kubwa ya kufika kwenye Halmashauri hizo za Wilaya ili kuweza kupata huduma za kijamii. Je, Serikali haioni haja ya kusisitiza jambo hili la kupata Wilaya mpya ya Ukonga? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mheshimiwa Silinde, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza Mheshimiwa Mbunge anasema mchakato ulifanyika mwaka 2015, wakati wa mchakato ule Halmashauri za Ubungo na Kinondoni ndizo zilizokuwa na sifa za kupata Halmashauri za Wilaya na anasema twende tuka-review mchakato wa mwaka 2015. Nafikiri jibu la Serikali ni la msingi, kama kuna maombi mapya ni lazima muanze upya mchakato na kila kipindi kinapopita kinakuwa na sababu zake. Kwa hiyo, maombi yote ya nyuma kwa sasa hivi tunasema ni maombi ambayo hayatambuliki kwa sababu zoezi lile lilifanyika kwa wakati mmoja na halmashauri ambazo zilikidhi vigezo zilipewa hiyo hadhi za kuwa wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ushauri wangu utabaki palepale kwamba kama kuna nia hiyo anzeni upya watu wa Ukonga mfuate taratibu zote za kisheria, mlete maombi na sisi tutayapeleka kwa Mheshimiwa Rais. Rais ndiye atakayekuwa na maamuzi ya mwisho ya kuanzishwa *either* kwa Wilaya ya Ukonga ama kusitisha kwa kadri atakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la pili amerudia jambo lilelile kwa sababu Makao Makuu ya Ofisi za Jiji yapo mjini sana na anaona kwamba kuna haja ya kuwa na wilaya mpya ili kusogeza huduma. Kikubwa ni kwamba Serikali tutaendelea kupeleka huduma kwa wananchi, lakini hayo maombi yenu kama yatakidhi basi Serikali itaendelea kuangalia. Hilo nafikiri ndiyo jibu sahihi kwa wakati huu. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, swali la nyongeza.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kuniona. Kwa kuwa Makambako kuhusiana na masuala ya Polisi na *TANESCO* ni wilaya na taasisi zingine ni wilaya. Serikali haionsi sasa ni muhimuMakambako tupewe wilaya kwenye Halmashauri ya Mji wa Makambako kwa sababu taasisi zingine zote zipo kiwilaya kasoro halmashauri kutamka kwamba ni Halmashauri ya Wilaya ya Makambako?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deo Sanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge ameeleza kwamba Halmashauri ya Mji wa Makambako ambapo yeye ndiye Mbunge wa eneo hilo kwamba kipolisi ni wilaya. Nieleze tu kuna wilaya za kipolisi na wilaya za kiutawala ambapo sisi Ofisi ya Rais - TAMISEMI tunasimamia. Ndiyo maana unajikuta kuna maeneo mengine ni Mikoa ya Kipolisi, kwa mfano llala ni Mkoa, lakini ni wilaya, kulikuwa na Kinondoni wakati fulani zilikuwa Wilaya za Jiji la Dar es Salaam wakati ule lakini bado zilikuwa zinatambulika kama ni Mikoa ya Kipolisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, huwezi kuniambia tu kwa sababu Kinondoni ni Mkoa wa Kipolisi basi tutamke leo kutakuwa na Mkoa wa Kinondoni. Niseme tu hizo ni taratibu za kiutendaji za kiserikali endapo wao wanaona wanahitaji kuwa na halmashauri basi wafuate taratibu kama ambavyo tumejibu katika swali la msingi. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini wakati wa ugawaji wa hizi wilaya mpya ama halmashauri mpya ni vizuri maombi yakishakuja mnapoenda kujiridhisha mtazame jiografia ya maeneo hayo. Nasema hivyo kwa sababu kuna changamoto, yaani lile lengo la kusogeza huduma kwa wananchi linakuwa halitimii. Mfano mzuri ni Wilaya ya Mbeya ambayo ina halmashauri mbili; kuna Jiji halafu kuna Mbeya Vijijini.

Sasa Mbeya Vijijini inaizunguka Mbeya Mjini maana yake mtu ili akapate huduma lazima apite Mbeya Jiji aende huko yaani kila kona unayopita, sasa Mbeya Vijijini imejikuta kimsingi inapakana na wilaya zote za Mkoa wa Mbeya, kwa hiyo, mtu anazunguka sana. (*Makofii*)

Sasa ni vizuri wakati wa kujiridhisha muangalie jiografia ili maeneo yagawiwe kwa namna ambayo mtu anasogezewa huduma kama ambavyo linakuwa ni lengo lenu. Pengine ni muda sasa wa kuziondoa kabisa sababu za kisiasa za kugawanya haya maeneo ndiyo maana tunajikuta maeneo mengine ni madogo sana, mengine ni makubwa sana, kunakuwa hakuna ule uwiano wa kutoa huduma. (Makofi)

Mheshimiwa Alaudin Hasham Salim, Mbunge wa Ulanga, sasa aulize swali lake.

Na. 487

**Ukosefu wa Dawa na Vifaa Tiba katika Vituo vya kutolea
Huduma za Afya Wilayani Ulanga**

MHE. SALIM A. HASHAM aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua changamoto ya ukosefu wa dawa na vifaa tiba katika vtuo vya kutolea huduma za afya Wilayani Ulanga?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA
SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salim Alaudin Hasham, Mbunge wa Jimbo la Ulanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuboresha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba kwa kuongeza bajeti katika Wilaya ya Ulanga na nchini kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya dawa katika Halmashauri ya Wilaya Ulanga imeongezeka kutoka shilingi

milioni 337.49 (Serikali Kuu, fedha uchangiaji huduma na Mfuko wa Pamoja wa Afya) mwaka 2015/2016 hadi shilingi milioni 475.53 mwaka 2020/2021. Upatikanaji wa dawa muhimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga umeongezeka kutoka asilimia 68 mwaka 2015/2016 hadi kufikia asilimia 82.2 mwaka 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada hizi bado kuna changamoto ya upungufu wa baadhi ya dawa na vifaa tiba vituoni. Serikali itaendelea kuboresha bajeti na usimamizi wa bidhaa hizi ili kuondoa changamoto hiyo.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Salim Alaudin Hasham, swali la nyongeza.

MHE. SALIM A. HASHAM: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, je, Waziri yupo tayari kutembelea baadhi ya zahanati, vituo vya afya pamoja hospitali ya wilaya ili kujiona changamoto hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali la pili, kwa kuwa upungufu wa watumishi katika jimbo langu umefikia asilimia 67, je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza watumishi wa afya katika Jimbo la Ulanga? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mheshimiwa Silinde, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali madogo mawili ya Mheshimiwa Salim Alaudin Hasham, Mbunge wa Jimbo la Ulanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza ni kama ombi, je, tupo tayari kutembelea jimbo lake na kujiona

changamoto hizo zinazolikabili. Nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge tupo tayari mimi na mwenzangu Naibu Waziri wa TAMISEMI anayeshughulikia masuala ya afya Mheshimiwa Dkt. Dugange na tutafika katika eneo lake na kushuhudia haya ambayo ameyazungumza na tutachukua hatua za kimsingi kuwasaidia wananchi wa jimbo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali la pili, ameuliza kama tupo tayari kuongeza watumishi. Niseme tu kwa kadri tutakapokuwa tunaendelea kupata kibali cha kuajiri kutoka Ofisi ya Rais – Utumishi tutaendelea kuajiri na kuongeza watumishi. Kwa hiyo, katika nafasi chache tunazopata kama ambazo tunakwenda kuzajiri nafikiri kabla ya mwisho wa mwezi huu tutakuwa na watumishi kwenye kada ya afya karibu 2,700. Kwa hiyo, mionganoni mwa watumishi hao wengine tutawaleta katika jimbo lako ili waweze kusaidia kuongeza ile ikama ya watumishi wa kada ya afya. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Kajege swali la nyongeza.

MHE. CHARLES M. KAJEGE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Tatizo walilonalo Ulanga ni sawasawa na tatizo tulilonalo katika Wilaya Bunda hasa katika Jimbo la Mwibara. Je, ni lini Serikali itatusaidia kuondoa tatizo la madawa na vifaatiba katika zahanati zetu?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mheshimiwa Siliinde, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA ((MHE. DAVID E. SILINDE)): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Kajege, Mbunge wa Mwibara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, anachouliza Mheshimiwa Mbunge ni lini Serikali sasa tutasaidia kuondoa tatizo la vifaatiba na dawa katika jimbo lake. Ukiangalia katika bajeti za Serikali kila mwaka tumeendelea kuongeza fedha ili kuhahakisha tunasogezza huduma hizi kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri, sisi wote ni mashuhuda bajeti ya vifaatiba na dawa kwa mfano katika mwaka 2015/2016 nchini ilikuwa ni shilingi billioni 31, lakini katika mwaka 2021/2022 tunazungumzia bajeti ya dawa na vifaatiba nchi nzima ni shilingi shilingi billioni 270. Kwa hiyo, niseme tu, tumeongeza bajeti tutaendelea kuongeza na kuboresha ili kuhakikisha tunaliondoa kabisa tatizo hili la huduma ya afya katika maeneo yetu yote nchini. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Agnesta Lambert, swalii la nyongeza.

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuuliza swalii dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukosefu wa dawa na vifaatiba imekuwa ni changamoto karibia nchi nzima. Je, ni kwa nini Serikali basi isihamasishhe uwekezaji mdogo na mkubwa wa viwanda vyta dawa na vifaa tiba ikiwa ni pamoja na kuondoa Kodi ya Forodha pamoja na masharti mengine ili basi viwepo viwanda vingi ambapo mwisho wa siku dawa hizi zitakwenda kuwasaidia Watanzania na hususani walio wengi huko vijijini?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Agnesta Lambert ameleta pendekezo kwamba ni kwa nini sasa Serikali isione haja ya kuongeza uwekezaji kwenye viwanda vyta kuzalisha dawa na vifaa tiba nchini ili kupunguza hii adha? Jambo hili ni jema, ndiyo maana sasa hivi sera ya Serikali ni kuhimiza watu wote wanaotaka kuwekeza nchini waje, ikiwemo kwenye sekta hii ya dawa na vifaa tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi tunawaruhusu watu wote na katika kipindi sahihi kabisa cha kuwekeza ni

sasa, kwa sababu Serikali imeboresha mazingira bora ya kufanya biashara nchini ambayo yanaruhusu wawekezaji wote kuwekeza ndani ya nchi. Ninaamini hao watakaokuja kuwekeza kwenye maeneo ya dawa na vifaa tiba wanapewa kipaumbele zaidi. Kwa hiyo, mazingira ya Serikali yako sahihi na tunawaruhusu na Serikali itaendelea kuwekeza zaidi. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kasalali Mageni, swali la nyongeza.

MHE. KASALALI E. MAGENI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa bajeti ya dawa ya Serikali imeongezeka kama ambavyo taarifa zinaonesha kutoka shilingi bilioni 31 mpaka shilingi bilioni 270 na kwenye makabrasha ya Serikali inaonekana upatikanaji wa dawa umeongezeka kwa kiwango kikubwa lakini uhalisia kwenye Vituo vya Afya na Zahanati siyo sawa na hizi taarifa kwa sababu bado kwenye Jimbo la Sumve katika Vituo vya Afya na Zahanati tatizo la upatikanaji wa dawa bado ni kubwa sana:- (*Makofii*)

Je, Wizara haioni sasa umefika wakati muafaka wa kutengeneza utaratibu mahususi ambao utaisaidia Serikali kwenda kutatua tatizo hili kwa uhalisia kwa kupata taarifa halisi kutoka kwenye vituo na siyo makabrasha ambayo yanapatikana kwa wataalam? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Kasalali Mageni amesuggest jambo jema ambapo ukiangalia katika hotuba ya Wizara ya Afya wakati wanaisoma hapa pamoja na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwenye Idara ya Afya ambayo sisi tunasimamia, katika moja ya changamoto ambayo imekuwa ikitukumba ni kwamba Serikali imekuwa ikipeleka dawa lakini haziwafikii walengwa kama ambavyo imekusudiwa. Sababu

kubwa ilikuwa ni baadhi ya watumishi, sio wote, kutokuwa waaminifu; aidha kwa kuza zile dawa ama wengine kutokuzitumia mpaka zina-expire, matokea yake wale wagonjwa wanaotakiwa wapatiwe zile huduma za kimsingi wanashindwa kuzipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sasa hizi Serikali tuko katika hatua za mwisho za kuandaa mfumo ambao sasa hivi utakuwa unajua dawa inayoingia na dawa inayotoka kiteknolojia. Kwa hiyo, naamini hiyo ndio itakuwa mojawapo ya suluhisho la kuondoa hii changamoto iliyopo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay Mbunge wa Mbulu Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 488

**Kugawanya Rasilimali za Halmashauri ya Wilaya
ya Mbulu na Mji wa Mbulu**

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatoa uamuzi wa mwisho wa mapendekezo ya mgawanyo wa rasilimali, madeni, majengo, watumishi na mashamba kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu na Halmashauri ya Mji wa Mbulu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Silinde majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA
SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu katika swalii Na. 116 tarehe 12 Januari, 2021 mgawanyo wa rasilimali watu, magari, pilkipiki, rasilimali na madeni kati ya Halmashauri ya Mji Mbulu na Halmashauri ya Mbulu umefanyika kwa asilimia 100 kwa kuzingatia mwongozo wa ugawaji wa mali na madeni ulioandaliwa na Ofisi ya Rais TAMISEMI wa Mwaka 2014. Katika mgawanyo huo Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu kwa maana ya Halmashauri mama, ilipata asilimia 60 na Halmashauri ya Mji wa Mbulu ilipata asilimia 40.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zacharia Paulo Issay swalii la nyongeza.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo ya nyongeza. Kwa kuwa mgawanyo huu ulifanyika mwaka 2015/2016, ni miaka mitano, sita sasa; na kwa kuwa hadi sasa hakuna tamko la wazi la Wizara kuwasilishwa mbele ya Mabaraza ya Madiwani wa Halmashauri zote mbili ili kuondoa hali ya madeni mbalimbali na rasilimali nyingine na mkanganyiko uliopo:-

Je, ni lini sasa Wizara itawasilisha mgawanyo huu kwa waraka maalum wenye *GN* mbele ya Mabaraza hayo mawili? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, kwa kuwa katika mgawanyo wa rasilimali tulizopokea ni pamoja na watumishi; Halmashauri ya Mji Mbulu sasa inakabiliwa na upungufu mkubwa sana wa watumishi takribani miaka sita sasa kwa ajili ya hizo asilimia 40 ambapo wengine wamestaifu na wengine wamefariki kwa sababu mbalimbali:-

Je, lini sasa Serikali itaondoa tatizo hili la upungufu wa watumishi hawa angalau kwa awamu katika sekta mbalimbali katika Halmashauri yetu ya Mji wa Mbulu? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa David Silinde, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Zacharia Paul Issaay katika swali lake la kwanza alikuwa tu anataka kwamba kujua ni lini Serikali itatoa tamko la wazi ambalo litawasilishwa katika mabaraza ili kutoa waraka maalum ili hizi Halmashauri mbili ziweze kujua sasa zimeshagawanyika rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu, kwa sababu jambo hili limefanyika muda mrefu, ninaiagiza Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwamba waandike hili tamko la wazi haraka iwezekanavyo na ndani ya miezi mitatu jukumu hilo tutakuwa tumeshalifanya na mabaraza hayo mawili yatakuwa yamekaa ili wawe wanajua kabisa rasmi wameshaganyika. Kwa hiyo, ndani ya miezi mitatu tutakuwa tumeshalitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, ni kero ya watumishi wachache katika eneo lake na anataka kujua Serikali itatataua lini tatizo hili; niseme tu Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora, tutashirikiana kwa Pamoja, kwa sababu wanaotoa kibali cha kuajiri watumishi ni Ofisi ya Raisi Utumishi na Utawala Bora na sisi jukumu letu ni kupata hao watumishi na kuwapangia vituo na maeneo ya kwenda kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wale ambao tunaendelea kuajiri kama ambavyo tumekuwa tukiendelea kuajiri walimu, tumekuwa tukiendela kuajiri watumishi katika kada ya afya, tunaendelea kuwaleta katika Halmashauri zetu nchi kwa kadri tutakavyokuwa tunapata kulingana na kibali tunavyopewa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Kwa hiyo, niseme tu kwamba Mheshimiwa Mbunge tutaendelea kuleta watumishi katika eneo lako kwa kadri tutakavyokuwa tunapewa kibali na bajeti ya Serikali inavyohitaji. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa

kuwa mgawanyo wa Halmashauri hizi mbili ultangazwa kwenye *GN* ya mwaka 2015, kwa nini sasa ichukuwe miezi mitatu wakati tangazo liko wazi na sheria hii iko wazi sana?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa David Ernest Silinde, Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Flatei Massay ameeleza kwamba *GN* ni kweli ilitoka mwaka 2015 lakini bahati mbaya sana tamko la wazi lilicheleweshwa kuwasilishwa. Kwa hiyo, nikiri kabisa kwamba nafikiri kulikuwa na kupitiwa kwenye utekelezaji wa jambo hili na ndiyo maana, kwa sababu Serikali ya Awamu ya Sita tuko hapa, tumeahidi kulitekeleza ndani ya miezi mitatu ili kuhakikisha jambo hili limeisha kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Chaurembo swali la nyongeza.

MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa mgawanyo wa mali iliyokuwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam haukuhusisha wadau wakiwepo Waheshimiwa Wabunge:-

Je, Serikali haioni sasa haja ya kuu-review ule mgao hasa katika ile mikopo ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu?

NAIBU SPIKA: Nataka kuamini ukisema Wabunge, unamaanisha pia na Madiwani hawakushirikishwa. Kwa sababu kama walishirikishwa Madiwani halafu Wabunge ndio hamkuwepo, ni ninyi ambao hamkuwepo. Hebu fafanua kidogo.

MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, Mabaraza ya Madiwani wa Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam hayakushirikishwa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Jambo alilolita Mheshimiwa Abdallah Chaurembo ni kubwa sana ambalo linahitaji kwanza tufuatilie, tujiridhishe kwa sababu ninaamini kila jambo linapofanyika kunakuwa na muhtasari ambao huwa unaandikwa na vikao na idadi ya watu waliohuduria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, endapo jambo hilo halikufanyika, basi ninaamini Ofisi ya Rais, TAMISEMI itazingatia namna bora kabisa ambayo itasaidia jambo hili liweze kufanyika kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunalipokea na tutakwenda kulifanya kazi, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Janejelly Ntate, swali la nyongeza.

MHE. JANEJELLY J. NTATE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Maslahi yalikuwa ni hayo hayo ya Mkoa wa Dar es Salaam. Nashukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Wabunge wa Dar es Salaam, nataka kuamini hayo ni malalamiko ya Wabunge waliopita katika maeneo yenu, maana mgao haujafanyika kipindi hiki cha uchaguzi. Kwa hiyo, naamini mmepitia muhtasari mkaona Wabunge waliopita, hawakushirikishwa.

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, Mbunge wa Magu, sasa aulize swali lake.

Na. 489

Ujenzi wa Barabara ya Magu – Ng'hungumalwa

MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA aliuliza:-

Je, ni lini ujenzi wa barabara ya Magu – Ng'hungumalwa kwa kiwango cha lami utaanza baada ya upembuzi yakinifu kukamilika?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Msongwe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, Mbunge wa Magu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami, barabara ya Magu – Bukwimba - Ngudu – Ng'hungumalwa yenye urefu wa kilometra 71 ilikamilika mwaka 2019.

Katika mwaka wa fedha wa 2021/2022, Serikali imetenga shilingi milioni 1,500 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kilometra 10 kwa kiwango cha lami barabara hii. Serikali itaendelea na ujenzi wa barabara hii kadri ya upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Boniventura Kiswaga, swalii la nyongeza.

MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA: Mheshimiwa Naibu Spika, naridhika na majibu ya Serikali, kwa sababu safari moja huanzisha nyingine. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Serikali ilishapitisha ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Geita kwenda Nyang'hwale, tulikuwa tukipewa kilomita nne kila mwaka na sasa hivi tumeshajengewa zaidi ya kilomita name; miaka miwili iliyopita hatujapewa tena hizo kilomita nne nne:-

Je, Serikali inatoa kauli gani; imeifuta hiyo barabara kwa ujenzi wa lami au la?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mhandisi Msongwe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, alivyosema Mheshimiwa Hussein Amar Mbunge barabara ya Geita hadi Nyang'hwale ni barabara ambayo tayari imeshaanza kujengwa na Serikali hajaifuta barabara hiyo kujengwa kwa kiwango cha lami. Tumhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii itaendelea kujengwa kadri fedha itakavyoendelea kupatikana. Kwa hiyo, hajaifuta na haina mpango wa kuifuta, lakini itategemea na upatikanaji wa fedha hili kuendeleza ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Daniel Awack, swali la nyongeza.

MHE. DANIEL A. TLEMAI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa viongozi wakuu waliahidi kiwango cha kilimeta 10 katika Mji wa Karatu mwaka 2010 – 2015 na 2015 - 2020 mpaka leo hii hatuna hata kilometa moja: sasa ni lini ahadi ya viongozi wakuu itatekelezwa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Mhandisi Msongwe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Awack kuhusu ahadi za Viongozi wa Kitaifa ya kujenga barabara kilometra kumi katika Mji wa Babati, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kazi ya Serikali ni kujenga barabara hizo kama zilivyoahidiwa na Viongozi wa Kitaifa. Ujenzi huo kama ilivyoainishwa kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi zitajengwa katika awamu hii ya miaka mitano. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge avute subira na kadri bajeti itakavyoruhusu, hiyo barabara ya kilomita 10 itajengwa katika Mji wa Babati. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Shabani Shekilindi, swali la nyongeza.

MHE. SHABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Serikali imejiridhisha kuwa barabara ya kuanzia Dochti kuititia Ngulwi hadi Mombo ambayo ni kilometra 16 kuwa itajengwa na *TANROAD*:-

Je, ni lini barabara hiyo itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mhandisi Msongwe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Shekilindi barabara ya Dochti - Mombo yenye urefu wa kilomita 16 itajengwa na *TANROAD*, lakini katika mpango huu kwa mwaka huu wa bajeti, barabara hii haimo. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba *TANROAD* kuititia Serikali, barabara hii katika mipango ijayo itajengwa kama ilivyoahidiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Innocent Bilakwate, swali la nyongeza.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Barabara ya Murushaka kwenda mpaka Mrongo ni barabara ya kiuchumi kwa Mkao wa Kagera, lakini pia ni barabara muhimu inayounganisha nchi ya Tanzania na Uganda; na kwa umuhimu wake Mheshimiwa Hayati Pombe Magufuli aliahidi ijengwe kilometa 50 za haraka. Ni lini kilometa 50 hizi zitajengwa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mhandisi Msongwe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli barabara ya Mrongo yenye urefu wa kilomita 112 aliyoitaja Mheshimiwa Bilakwate ni kweli iliahidiwa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, barabara hii imeingizwa kwenye mpango na fedha imetengwa kwa ajili ya kuanza mwaka wa fedha ujao kwa kiwango cha lami. Nadhani tumetenga kama siyo chini ya shilingi bilioni tatu kwa kuanzia. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa wa Kyerwa na wananchi wa Kyerwa, ahadi ya Mheshimiwa Rais Hayati itaanza kutelekezwa mara tutakapoanza utekelezaji wa bajeti ambayo Bunge lako imelipitisha. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu kutoka kwa Wabunge na majibu kutoka upande wa Serikali. Sasa kwa kawaida huwa tunamaliza saa nne, lakini Kanuni zetu zinatoa mwongozo wa maswali mangapi Waziri anaweza kuulizwa ya nyongeza. Kwa hiyo hiyo ndiyo changamoto tuliyonayo na Kanuni tumejiwekea sisi wenywewe.

Sasa ninalo tangazo moja hapa, matangazo ya wageni hayajaja bado, lakini naona wageni wako wengi na kabla sijatoa hili tangazo nitoe ufanuzi kidogo.

Mheshimiwa Chaurembo, Mbunge wa Mbagala, ametoa maelezo ya ziada, kwamba mgao anaousema hauna uhusiano na mgawanyo wa zile halmashauri ama wilaya Dar es Salaam, isipokuwa ni mgawanyo baada ya kuvunjwa kwa Jiji la Dar es Salaam na kubaki wilaya moja ile ya llala. Kwa hiyo Mheshimiwa Naibu Waziri, utakapokuwa unakwenda kufuatilia kama ulivyosema, unakwenda kufuatilia mgawanyo baada ya kuvunjwa kwa Jiji la Dar es Salaam.

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge; anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba leo, Siku ya Alhamisi, tarehe 24, Juni, 2021, kutakuwa na semina kwa Wabunge wote itakayofanyika katika Ukumbi wa Pius Msekwa kuanzia saa saba mchana. Semina hiyo itaendeshwa na *Tanzania Sports Betting Association*. Waheshimiwa Wabunge wote mnatakiwa kuhudhuria.

Sasa hili tangazo liko tofauti kidogo na matangazo mengine kwa sababu mengine huwa Waheshimiwa Wabunge mnakaribishwa kuhudhuria, leo Waheshimiwa Wabunge mnatakiwa kuhudhuria na Mheshimiwa Spika. Kwa hiyo tutakapositisha shughuli za Bunge hapa, Wabunge wote tunatakiwa kuelekea Msekwa.

Baada ya ufanuzi huo na tangazo hilo, tutasubiri tangazo la wageni, tutawatangaza litakapokua. Kwa sasa tutaendelea na ratiba yetu.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Cecil David Mwambe.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nimesimama kwa Kanuni ya 53(4) kuhusu kujibiwa maswali kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri anajibu swali langu leo ndani ya Bunge, naomba kurekebisha kwamba majibu aliyo yatoa ni sahihi kabisa lakini hayahusiani na swali langu, kwa sababu swali langu linahusu Jimbo la Ndanda ambalo liko Halmashauri ya Wilaya ya Masasi *DC* au Vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, majibu aliyo yatoa ni sawasawa lakini yako Masasi Mji, kwa sababu Masasi *DC* na Masasi Mji kuna baadhi ya vijiji vinafanana kiasili kwa maana ya majina. Kwa mfano Kijiji cha Sululu kipo Masasi Mji, Kijiji cha Sululu ya leo kipo Masasi Wilaya (Vijiji); Kijiji cha Chipunda kipo Masasi Vijiji lakini pia kipo kwenye Kata ya Mkululu Masasi Mji. Kwa hiyo hivyo vijiji ni kweli vina namba, kama ambavyo ameelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nililiza kuhusu vile vijiji ambavyo vipo upande wa Jimbo la Ndanda ambavyo havina namba. Sasa naomba mwongozo wako kwamba ikikupendeza, swali hili basi lifanyiwe tena utaratibu wa kuweza kupata majibu. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ameomba Mwongozo Mheshimiwa Cecil Mwambe na Kanuni yetu ya 53 inataka maswali yajibiwe kikamilifu. Nadhani wakati majibu yakitolewa hapa na Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Mbunge aliposimama alieleza kwamba vijiji vilivyotajwa kwenye majibu viko sahihi na taarifa pia ziko sahihi, isipokuwa vipo vijiji kwenye Jimbo lake la Ndanda ambavyo vina majina hayo ambayo ameyataja ambavyo ndio alitaka majibu kuhusu vijiji hivyo.

Sasa majibu ambayo Serikali imeleta ni majibu ambayo yanatoka jimbo lingine hata kama baadhi ya vijiji hivyo vinafanana majina, lakini Mheshimiwa Mbunge swali lake lilikuwa linahusu vijiji vilivyo na majina hayo kwenye jimbo lake. Wakati Naibu Waziri akitoa majibu nililekeza kwamba swali hilo lijibiwe upya kwa kupata taarifa kutoka kwenye Jimbo la Ndanda.

Kwa hiyo Mheshimiwa Cecil Mwambe kwa kuomba kwake mwongozo alitaka kujua sasa kama hilo jambo linachukuliwaje. Majibu ni hayo, kwamba swali lako Mheshimiwa Cecil Mwambe linajibowi upya. Kwa hiyo Serikali italeta majibu, halafu litasomwa na utapata fursa ya kuuliza maswali ya nyongeza wakati huo. Kwa hiyo Serikali ilete majibu Ofisi ya Maswali hapa Bungeni halafu litapangiwa siku maalum.

Waheshimiwa Wabunge, limekuja pia tangazo la wageni waliopo humu ndani siku ya leo.

Tutaanza na wageni wawili wa Mheshimiwa Spika ambaao wanatoka Kampuni ya *Pink Diamond* kutoka Jijini Dar es Salaam na hawa ni Ndugu Zukrah Mattembe ambaye ni Afisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya *Pink Diamond*; karibu sana Zukrah Mattembe. Sijui kama Mheshimiwa Mattembe humu ndani wana uhusiano, lakini kuna Mbunge humu anaitwa Mheshimiwa Aysharose Mattembe. Ahsante sana na karibu sana. (*Makofi*)

Ameongozana na Ndugu Suhayla Salum ambaye ni Mkurugenzi wa Uendeshaji Kampuni ya *Pink Diamond*. Karibu sana. Naona kwa kwezi hawa wanatoka *Pink Diamond* kwa namna walivyopendeza, naona wanawatia moyo vijana wetu wanaojishughulisha na ushonaji; karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni 70 wa kwangu ambaao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma na hawa ni mabinti wanaoandaliwa kushika nafasi za uongozi mbalimbali katika nchi, wanaitwa Binti Makini, wakiongozwa na Roselinda Mrase. Karibuni sana mabinti wetu. (*Makofi*)

Jamani, sijaauliza umri wao lakini hawa ni mabinti wanaojiandaa kushika nafasi mbalimbali, kwa hiyo Wabunge pia humu ndani maana yake tukae sawa, wako tayari kwa ajili ya kuja kuchukua nafasi mbalimbali humu ndani. Hata hivyo, nataka kuamini hawana mpango wa kuchukua ya kwangu. Ahsanteni sana, sasa mnaweza kukaa. Karibuni sana. (*Makofi/Kicheko*)

Tunao pia wageni watatu ambao nao ni wageni wangu; mmoja wao ni mwandaaji wa *The Mboni Show*, Ndugu Mboni Masimba, ambaye ameambatana na watoto yatima. Sasa huyu ameambatana na watoto yatima kutoka Kituo cha Amani na Kituo cha Safina ambao ni washindi wa Bonanza la Watoto Yatima na hawa ni Ndugu Siraji Daud na Ndugu Aliya Abdallah; karibu sana. (*Makof!*)

Kabla hamjaka, Waheshimiwa Wabunge, Ndugu Mboni Masimba amekuja na hawa watoto hapa, walishinda hilo *bonanza* na watapata fursa ya kusafiri kwenda Uturuki, watasafiri na Mboni Masimba. Kwa hiyo hii nadhani ni picha nzuri, kwamba watoto yatima wasiwe wanakata tamaa, lakini watu wote tunaoweza kuwasaidia watoto yatima basi tuwasaidie ili na wao wasijisikie vibaya kwa kupoteza wazazi wao katika umri mdogo. Tunakupongeza sana Mboni Masimba kwa kazi nzuri unayofanya ya kuwasaidia watoto hawa wajisikie vizuri. (*Makof!*)

Sasa nataka kuamini siyo tu kwamba watakwenda Uturuki, warudi halafu basi, nataka kuamini na masomo yao hivi yatatazamwa pia hawa watoto wawili kama washindi, kwamba utaendelea kuwahudumia mpaka wafanye vizuri katika masomo yao pia. Tunawatakia kila la heri watoto wetu wazuri, karibuni sana Bungeni. Pia tunawatakia safari njema ya Uturuki na mkajifunze huko muwe watoto wazuri na msikate tamaa na ninyi muwatlie moyo watoto wengine, kwamba wanaweza kuwa chochote wanachotaka. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni mbalimbali pia wa Waheshimiwa Wabunge walioko hapa. Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Mussa Zungu ambao ni wataalam wa *IT* kutoka Ilala, Jijini Dar es Salaam na hawa ni Ndugu Ally Makame na Ndugu Hamis Hamza. Karibuni sana vijana kutoka Ilala.

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro ambaye ni Waziri wa Maliasili na Utalii ambao ni shemeji zake kutoka Songea, Mkoani Ruvuma, wakiongozwa na Dkt. Ester Elisaria. Karibuni sana. Sasa hapa wameandika

shemeji zake, tukawa tunasubiri tuone kundi, lakini naona uko mwenyewe shemeji yake Mheshimiwa Waziri; karibu sana. (*Makof*)

Ahaa! Wote hao ni shemeji zake? Haya jamani. Mimi siyo mtani wa Wangoni, kwa hiyo sitaki kuongea mambo hapa mbele. (*Makof*)

Wageni 40 wa Mheshimiwa Selemani Jafo ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, ambao ni wapigakura wake kutoka Jimbo la Kisarawe wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM, Wilaya ya Kisarawe Ndugu Khalfan Sika. Karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Selemani Jafo. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni watano wa Mheshimiwa Profesa Shukrani Manya ambaye ni Naibu Waziri wa Madini na hawa ni majirani zake kutoka Jijini Dodoma, wakiongozwa na Ndugu Tulibako Minga. Karibuni sana. (*Makof*)

Tunao wageni 39 wa Mheshimiwa Ummey Nderiananga ambaye ni Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughullikia masuala ya Watu Wenye Ulemavu, ambao ni Mwenyekiti wa Shirikisho la SIVYAWATA, Diwani na Viongozi wa Vyama mbalimbali vya Watu Wenye Ulemavu, wakiongozwa na Mheshimiwa Ernest Kimaya. Karibuni sana ndugu zetu, tumefurahi kuwaona. Mheshimiwa Ummey Nderiananga, mwakilishi wenu, anafanya kazi nzuri sana. karibuni sana Bungeni. (*Makof*)

Tunao pia wageni 16 wa Mheshimiwa *Engineer Maryprisca Mahundi* ambaye ni Naibu Waziri wa Maji na hawa ni vijana wa itifaki Mkoa wa Mbeya, wakiongozwa na Ndugu Twalib Belege. Karibuni sana vijana kutoka Mkoa wa Mbeya, wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji. (*Makof*)

Tunao pia wageni sita wa Mheshimiwa Janejelly Ntate ambao ni Viongozi wa Chipukizi kutoka Temeke, Jijini Dar es

Salaam, wakiongozwa na Ndugu Akbar Ngemera. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni 20 wa Mheshimiwa Boniphace Butondo ambao ni wanachuo kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, wakiongozwa na Ndugu Renatus Makolo. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni 21 wa Mheshimiwa Joseph Mkundi ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotoka Ukerewe, Mkoani Mwanza, wakiongozwa na Ndugu Frank Pachal. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava ambaye ni mpigakura wke kutoka Mkoani Shinyanga na huyu ni Ndugu Daudi Sahani. Sijui amekaa upande gani huyu, haya, karibu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, huyu aliiingia kukupigia kura huyu? Haya karibu sana Ndugu Daudi Sahani, maana sasa ameanza kutupa wasiwasi humu ndani kama huyu ni mpigakura.

Wageni wanne wa Mheshimiwa Noah Lemburis ambao ni Madiwani na mke wa Mbunge kutoka Arumeru Mkoani Arusha, wakiongozwa na mke wake, Ndugu Thabea Noah. Karibuni sana. Hebu mke asimame, ndio yupi hapo? Karibu sana. jamani huyo ndio wifi yetu na shemeji yetu wengine. (*Makofi*)

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Daniel Awack ambaye ni mpigakura wake kutoka Karatu, Mkoani Arusha na huyu ni Ndugu Cornelia Isdory. Karibu sana. (*Makofi*)

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Josephine Genzabuke ambao ni ndugu zake kutoka Mkoani Kigoma wakiongozwa na Ndugu Josephine Ntauheza. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Kasalali Mageni ambaye ni binamu yake kutoka Ksimba, Mkoani Mwanza na huyu ni Ndugu Renatus Kwiyukwa. Karibu sana. (*Makof*)

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana wakiongozwa na Ndugu Penina Mwinuka. Sijui wamekaa upande gani hao; karibuni sana. (*Makof*)

Tunao wageni walitembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Kundi la kwanza ni wageni 15 ambaao ni Wajumbe wa Chama cha Netiboli kutoka Wilaya za Mkoa wa Dodoma ambaao wamekuja kujifunza namna Bunge linavyoendesha shughuli zake, wakiongozwa na Ndugu Elionora Mongi. Karibuni sana viongozi wa netiboli. (*Makof*)

Huyu Elionora Mongi, hebu simama. Jamani huyu kwa muda mrefu amekuwa Mwalimu wa *Bunge Queens*. Mkisikla *Bunge Queens* wamefanya mambo mazuri wakati wa michezo, basi mjue filimbi za huyu mama zimefanya kazi nzuri; karibu sana Bungeni, tumefurahi kukuona. (*Makof*)

Tunao pia wanafunzi 80 na Walimu kumi kutoka Shule ya Martin Luther ya Jijini Dodoma ambaao wamekuja kujifunza namna Bunge linavyoendesha shughuli zake, wakiongozwa na Mwalimu Paulo Silla. Karibuni sana Bungeni, tumefurahi kuwaona na tuwapongeze tena kwa kuitikia wito wa Mheshimiwa Spika. Walimu tunawapongeza kwa kuwaleta wanafunzi. Mheshimiwa Spika alitoa wito kwamba wanafunzi wawe wanakuja kujifunza humu na sisi tunafurahi tukiwaona. Karibuni sana watoto wetu na tunawatachia kila la heri katika masomo yenu. (*Makof*)

Sasa hapa nilikuwa naijiliza, Profesa Kishimba ule mchango wake wa kucaa mashati meupe, sijui amekaa upande gani, lakini naamini Serikali inaona kwamba wanafunzi wanaweza kusoma hata wasipovaa mashati meupe.

Baada ya kusema hayo, matangazo yangu yamekwisha, tunaendelea na ratiba iliyo mbele yetu. Katibu.

NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2021
(The Finance Bill, 2021)

(Majadiliano Yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Majadiliano yanaendelea Waheshimiwa Wabunge na hapa ninayo majina ya Waheshimiwa Wabunge walioomba kuchangia. Tutaanza na Mheshimiwa Jumanne Sagini, atafuatiwa na Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas na Mheshimiwa Zaytun Seif Swai ajandae.

MHE. JUMANNE A. SAGINI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuzungumza kwa ufupi kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha na mapendekezo yaliyoletwa na Serikali ili kuridhiwa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, niishukuru Serikali na hapa nadhani Wabunge tukubaliane kwamba katika Muswada huu kwa sehemu kubwa sana Serikali wamekuwa wasikivu. Ukiangalia kwa makini mambo mengi ambayo yamelalamikiwa sana katika Bunge liliopita na hata mwanzo mwa Bunge hili, yamefanyiwa kazi kubwa sana kwenye hotuba ya bajeti na yanaonekana kuwa *reflected* vizuri sana kwenye mapendekezo haya ya Muswada wa Sheria ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo mengine pengine ni sintofahamu ya baadhi tu ya watu, hata niliona mijadala mingine jana na pengine juzi, ni sintofahamu inayotokana na uelewa tu ambao nadhani ukifanuliwa vizuri tunaweza tukakubaliana kwamba hatua hizo bado ni njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano, marekebisho yaliyofanyika yaliyo mengi yanalenga kuboresha maeneo ambayo Wabunge tumelalamikia. Mtaona hata hii *PAYE* imeshushwa kutoka asilimia tisa kwenda asilimia nane, lilikuwa

ni jambo la muda mrefu. Iliwahi kuwa *double digits*, tangu Serikali ya Awamu ya Nne, ikashushwa kidogo, ikashushwa tena Awamu ya Tano ikaenda kwenye *single digit*, naona Awamu ya Sita pia imeendelea kushuka *single digit* kwenda asilimia nane.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo ni kuwapunguzia makali wafanyakazi, maana yake inavyoonekana wafanyakazi ndio ambao wamekuwa wakibeba mzigo wa kuendesha nchi yetu kupitia kodi kuliko maeneo mengine. Sasa angalau hii ya kupunguza inawapa nafuu wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika usikivu huo huo tuliona kuna lengo la kutoza asilimia 3 ya mapato kwa wachimbaji wadogo, lakini sema hawa ni wachimbaji wadogo hawaja-*graduate* wala mapato yao hayajajulikana vizuri unakwendaje kuwakata kodi asilimia tatu, lakini nalo naona Serikali imesikia imeliondoa, jambo jema sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jingine ambalo ni usikivu ule ule ambao Wabunge wengi tulichangia ni kwenye kodi za majengo. Tuliona huko nyuma imekusanywa na *TRA* changamoto zikaonekana, lakini sisi ambao tumefanya Sekta ya *TAMISEMI* tunapenda kuamini kwamba kodi za majengo ukisoma mapato ya asili ya *Local Government Authorities* huwa ni *property tax*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hapa miaka kadhaa iliyopita kodi hizi zilikuwa zinakusanya asilimia moja pamoja na Serikali Kuu, kwa usikivu ule ule tunaona imeamuliwa sasa fedha zitakusanywa kupitia *TANESCO*, lakini Serikali inazungumzia kuweka utaratibu wa kurejesha asilimia 15 kwenye Serikali za Mitaa ili waweze kuzitumia kuboresha mazingira yalipo majengo hayo, jambo jema hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa ungeniuliza hapa ningemshauri Mheshimiwa Dkt. Mwigulu hii ingeenda juu zaidi kwa sababu unapokusanya kodi ya majengo watu wanataka kuona kwenye mazingira yale ya majengo kwa kiasi gani yamekuwa bora, usafishaji, usoaji wa taka mijini, usafishaji wa

mitaro na kuiboresha pale inapokuwa imeharibika, mapato haya ndiyo ambayo kwa hiyo hata mwenye nyumba angeona analipa na thamani anaiona pale mbele ya nyumba yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunasema ni mwanzo mzuri wa kurejesha kiwango hiki, lakini matarajio yangu ni kwamba kiwango hiki kingepanda juu kingewasaidia sana *Local Government* kuwa na mapato ya uhakika zaidi. Lakini nafarijika alivyofafanua kwamba kwa wale ambao hawana mita za *LUKU* mfumo uliopo utaendelea kwa maana *Local Government* zjidhatiti kwa ajili ya kukusanya *property tax* kwenye majengo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni hili ambalo kidogo limeibua hisia la *transfer pricing* mimi nadhani kama hatua ambazo zinasemwa zilikuwa zinafanyika za kufilisi kabisa biashara, nadhani haikuwa na tija sana. Sasa hii inayopendekezwa si kuto adhibu badala yake ni kurekebisha adhabu ile kwa asilimia Fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa mawazo wangu na ningeomba Wabunge tuliunge hili mkono, kwamba madamu hatuende kumsamehe, lakini anakwenda kupewa adhabu isiyohusisha kufilisi kabisa, nadhani ni muelekeo mzuri zaidi kuliko kuzungumzia kwamba ulenge kufilisi halafu unafunga biashara hata wale watu waliokuwa wanlipa kutokana na biashara ile hawatalipa fedha hiyo wala hutaipata, mapato wala hutayapata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ambacho ningeomba Serikali ifanye ni kujenga uwezo wa watalaam wetu kubaini michezo ya *transfer pricing* kwa sababu ninavyojua hatuna watu wenye weledi huo, kwa hiyo, Serikali ingejizatiti kujenga uwezo wa watu wetu kwenye sekta hasa ya *TRA* na sekta yenyewe ya fedha ili kubaini vitu hivi kwa mapema zaidi kuliko...

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jumanne Sagini kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Constantine Kanyasu.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninampongeza mchangiaji Mheshimiwa Sagini, lakini dawa pekee ya *transfer pricing* ni kwa Serikali kusimamia vizuri sheria ya *Local Content* ambayo imeeleza vizuri kwamba katika mazingira ambapo *supplier* au mali inayotakiwa haipo Tanzania na *supplier* anatoka nje basi lazima huyo aingie ubia na mtanzania ili kuweza kuficha ile kitu, lakini kwa bahati mbaya imekuwa haisimamiwi. Nakushukuru sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jumanne Sagini unaipokea taarifa hiyo.

MHE: JUMANNE A. SAGINI: Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea, lakini haiondoi bado umuhimu wa kuendelea kujelimisha zaidi namna ya kubaini ujanja unaotumiwa na hawa wenzetu ili vijana wetu waweze kuyabaini mambo haya mapema na kuyadhibiti yanavyotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Tarimba. Mheshimiwa Zaytun Swai atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya.

Haya naambiwa hawa ni wajumbe wa Kamati ya Bajeti kwa hiyo wapo kwenye kamati, Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya, atafuatiwa na Mheshimiwa Michael Mwakamo, Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi ajiandae.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia. Kwanza nianzie kumshukuru tena Mwenyezi Mungu, lakini kwa namna ya pekee kabisa niendelee kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu

Waziri pamoja na wadau wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri iliyofanyika hasa katika kuangalia maeneo muhimu ambayo yakiboreshwa kuitia Muswada huu yatawezesha Taifa kukusanya mapato yaliyokusudiwa na kutekeleza miradi mbalimbali ambayo imekusudiwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo nilikuwa na michango michache katika baadhi ya maeneo. Ukienda katika sehemu ya tano nimetumia mchango ambao Mheshimiwa Waziri ulikuwa unawasilisha kwa ajili ya Muswaada huu.

Kwa hiyo ukichukua sehemu ya tano ambayo inahu sheria ya mikopo, dhamana na misaada sura ya 134 ambayo ulikuwa unapendekeza sasa kuongeza kifungu 13 (b) kitakachosaidia Serikari kuweza kutoa dhamana kwa kampuni ambayo itahitaji kukopa kwa kiwango kisichozidi asilimia ya hisa za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa napenda kujiridhisha zaidi na kushauri kwa sababu imeonekana katika uzoefu ulijitokeza katika miaka hii ya hivi karibuni baadhi ya dhamana hizi zimetumika vibaya, kwa hiyo nilikuwa nashauri, kwa sababu *CAG* sasa hivi amepata mamlaka ya kuweza kukagua makampuni ambayo Serikali ina hisa zaidi asilimia 50, basi nilikuwa nashauri hata pale Serikali inapokuwa imetoe dhamana kwa kampuni pamoja na kwamba ni kwa kiwango cha hisa zake basi *CAG* aweze pia kukagua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu gani? inawezekana tukaona pengine hisa zilizopo ni kiwango kidogo labda asilimia 20, lakini inaweza ikawa ni asilimia 20 ya mabilioni ya hela au matrillioni ya hela kulingana na mradi ulivyo, tuchukulie kama Mchuchuma na Liganga pale kuna fedha nydingi, sasa unaweza kukuta kwamba fedha kama hizo badala ya kutumika kwenye mradi husika nydingine zikatumika ndivyo sivyo. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri aidha tuongeze pale kwa *CAG* kwamba atatakiwa kukagua kwenye hisa hizo zinazozidi asilimia 50 pamoja na sehemu ambayo Serikali imeweka dhamana yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa pia naomba nichangie sehemu ya 24 kama ilivyorekebishwa kuhusu sheria ya kodi ya ongezeko la thamani sura 148(8) ambacho kinahusu kuondoa ongezeko la thamani kwa ajili ya vyumba vya baridi. Lakini imewalenga zaidi wauzaji wa mbogamboga, sasa nilikuwa nafikiri kwamba nila wale watu ambaao tunahitaji kuwainua wakiwemo wavuvi hata wanaohusika na masuala ya nyama kwa hiyo nifikirie pengine tusiwaangalie hao tu, tuangalie makundi hayo yote ili kuwezesha sasa hawa wananchi wetu kupata unaifuu katika uwekezaji wa vyumba vya ubaridi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile nilikuwa nashauri kwa upande wa mamlaka ya bandari kutenga *line* maalum inayohusika na bidhaa za aina hiyo kwa sababu wakati mwingine unakuta kwamba wanasubiri mpaka bidhaa hizo ziwe za kutosha ndipo ziweze kusafiri sasa bidhaa za mbogamboga au nyama au Samaki siyo sawa na chuma. Kwa hiyo, nafikiria kwamba ni vema sasa Mamlaka ya Bandari kuwezesha kabisa kuhakikisha kwamba bidhaa hizo au mazao hayo yanaweza kusafirishwa kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa pia napenda kuchangia kidogo kwenye eneo hili la, kwanza kwenye kuongeza idadi ya kutoza kodi kwa waajiriwa zaidi ya nne mpaka kumi, jambo hili limekuwa ni jema sana na linawezesha kusaidia uwekezaji hata katika maeneo ya vijijini. Lakini kubwa zaidi nimeshukuru kwa jinsi ambavyo tumeondoa kodi ya mafunzo kwa taasisi za kidini hususani hospitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda maeneo mengine kwa mfano kwenye Jimbo la Nyasa pale tuna hospitali ya Litui, tuna hospitali ya Liuli hayo maeneo yamekuwa ndiyo yakisaidia sana katika kupunguza changamoto za matibabu. Lakini sasa hivi kutokana na hizi gharama za kiuendeshaji na hivi Serikali sasa inavyokuwa imeanza tena kuangalia katika vituo vya afya vilivyojengwa na Serikali yenywewe katika maeneo sasa ni mbali na maeneo hayo unakuta kwamba hizo hospitali zimekuwa zinashindwa kujiedhesa kiasi

kwamba hata wale wananchi wanaoenda kutibiwa pale, kwa sababu walishajenga kichwani mwao kwamba sehemu ile ndiyo sehemu ya kuponea imekuwa kwa kweli wanapata changamoto kubwa na vifo hata vya wakinamama vimekuwa vikiongezeka, wakinamama inamaana kwenye kujifungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, jambo hili limekuwa ni msaada mkubwa sana na ninaomba kwa kweli tuzidi kuziangalia hospitali hizi ambazo zinatoa mchango mkubwa wa kipekee katika kuendelea kuisaidia Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya michango hiyo naendelea kuunga mkono hoja na ninaamini kwamba Sheria hii sasa ikishakuwa kamili itasaidia sana kuleta mabadiliko katika nchi yetu. Nazidi kumshukuru Waziri pamoja na Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi kubwa anayoifanya. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Michael Mwakamo, atafuatiwa na Mheshimiwa Kunambi, Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau, ajiandae.

MHE. MICHAEL C. MWAKAMO: Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru kunipa nafasi ya kuzungumza na kwa mujibu wa ratiba ya Bunge yawezekana ikawa ni mchango wangu wa kumaliza kwa Bunge hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na nianze kuchukua nafasi kwanza ya kuishukuru Serikali kwa namna bora ya bajeti ambayo umetuletea na mabadiliko haya ambayo wameleta mbele yetu ambayo leo tunayachangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya ya kumudu ya kukaa Bungeni kwa kipindi chote cha awamu ya kwanza na sasa natarajia kurudi jimboni kuendelea kupiga kazi na nani imani yangu wananchi wanatusubiri kuendelea na shughuli za maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno haya, nataka nitoe mchango wangu kwenye maeneo machache sana na hasa kwenye marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato sura 332 hasa kile kipengele namba 3 kinachozungumzia kodi ya zuio kwa kiwango cha asilimia mbili kwa mazao ya wakulima, wafugaji na wavuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejaribu kukitazama kieneo hiki, lakini nimejaribu kuangalia msingi wa hii tozo, lakini nikaona uzito ambao unakwenda kuwakuta hasa kundi la wafugaji ambalo nami nataka nilizungumzie kwa kina. Katika Bunge lote na hasa katika michango mbalimbali ya Wabunge waliotoa, tumejaribu kuona kundi la wafugaji la wavuvi na wakulima ni kundi ambalo linapata kiasi kidogo sana cha bajeti ya Serikali kuliko maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, na tumegundua ndiyo makundi ya wananchi ambao wapo kwenye kiwango cha chini sana cha umasikini, na lengo la Serikali ni kuhakikisha makundi haya yanakwenda kujiongezea kipato ili yaweze kuwa na maisha bora katika maeneo yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimekitazama kipengele hiki cha kodi cha asilimia 2 ambacho kimewekwa kwa ajili ya mazao ya mifugo Kilimo na Uvuvi, japo Serikali imezungumza kwamba hiki hakitawagusa wakulima moja kwa moja wadogo, lakini ukikiangalia kwenye kwenda kukitekeleza ni kwa asilimia kubwa sana wakulima hawa wadogo kitawagusa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema kitawagusa, nikizungumzia kwa mfano kwenye *panel* zima ya wafugaji, Kibaha vijijini niseme kwa mfano ninao wafugaji, lakini mpaka leo ninavyozungumza sijawa na chama cha ushirika cha wafugaji pale Kibaha vijijini. Vyama na umoja walionao chama cha ushirika pale Kibaha vijijini wao wanashughulika na suala zima la kujitengenezea miundombinu ya kupata huduma bora kwa mifugo yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hawana umoja ambao unafanya uweze kununua mazao ya mifugo ambayo wataweza kupeleka kwenye viwanda vikubwa na kuchakata. Kwa tafsiri hiyo sasa kwa sheria hii ilivyo maana yake sasa huyu mkulima mdogo ambaye atakosa kuuza atakuwa hana *AMCOS* au hana ushirika wa mifugo, maana yake atakosa soko la kuuza mifugo yake. Atategemea hawa tunaowaita mawakala mimi katika lugha nyepesi nawaita madalali, watalazimika kwenda kuchukua mifugo kwa wakulima kwa bei ya chini ili waweze kuzimudu hizi kodi zingine kuna matozo ambayo yametangulia kwenye mifugo kabla hii ya asilimia mbili. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mkulima huyu au mfugaji huyu akifikisha ng'ombe kwenye mnada uliowekwa na Serikali, ng'ombe mmoja anamlipia shilingi 3,000, lakini pia anamlipia shilingi 2,500 kumsafirisha kutoka mnadani kumpeleka anapotaka, mbuzi mmoja analipiwa shilingi 2,500 anakouzwa, halafu anamlipia shilingi 1,500 kumsafirisha kutoka hapo alipomnunua kumpeleka huko ambako anatakiwa akauzwe. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nikiitazama hii tozo inakwenda kutengeneza ugomvi kati ya wenyе viwanda ambao wanachakata mazao ya mifugo na wale mawakala, kwa sababu watakuwa mawakala wale watataka kupeleka mifugo pale na wale wenyе viwanda watahitaji kuwakata hiyo asilimia mbili kama kodi ya zuio waweze kupeleka Serikalini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nini kitatokea, kitakachotokea wale mawakala ambao ni wanunuzi wa kupeleka kwenye vile viwanda watashindwa kupeleka kwenye viwanda vyetu na watatoa mifugo hii nje kwa sababu ya kukataa kuilipa ile tozo ya asilimia mbili. Kwa sababu na wakishafanya hivyo viwanda vyetu hivi ambavyo tumevijenga ndani na katika hali ya kawaida kumbukumbu zangu nilizonazo na sijui kama watanirekebisha. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kipo kiwanda pale Kibaha ambacho ni *Tan Choice* na kingine kipo Longido, nchi nzima tuna viwanda hivi viwili ambavyo tunategemea wakachakate mazao yale ya mifugo. Sasa kwa tozo hii, maana yake kitakachotokea ni nini wale wauzaji wakubwa ambao wana nafasi ya kupeleka kwenye viwanda hivi wata-escape na kwenda pembezoni kwenda kuuza Kenya na kwingineko. Wakifanya hivyo mifugo yetu ya ndani itaendelea kununuliwa kwa bei ya chini na hawa watu wa kati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo jingine litakalotokea kwa kukosekana hawa watu kupeleka moja kwa moja mifugo kwenye viwanda vile, maana yake viwanda hivi pamoja vimewekeza kwetu havitapata malighafi, maana yake hawatazalisha na kama hawatazalisha litatokea tatizo la kukosa kutoa ajira ya kutosha kama ambavyo tuna lengo la wananchi hawa wapate ajira. Sasa nilikuwa ninaiomba Serikali iitazame vizuri hii kodi ya zuio, iitazame kwa makini sana kwa maslahi mapana ya wafugaji wetu wadogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na nalisema hili kwa sababu hawa wafugaji wadogo tena ukiangalia hivi viwanda vinavyochakata kwa mujibu wa utaratibu wa manunuzi, maana yake wanatakiwa wapokee mifugo sio moja kwa moja kutoka kwa hawa watu wafugaji wadogo kwa kitendo hicho maana yake bado wanalamizimisha mtu wa kati awepo, jambo ambalo nafikiri wangekiondoa hiki kwa sababu huyu mfugaji anachangia kwa kiasi kikubwa sana kwenye mfugo mmoja hadi anafika kwenye kuchakatwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ambalo nataka niliseme, Serikali ituangalie wengi Wabunge hapa tumezungumza kama kuna kundi ambalo linaishi pasipo kujitambua kwenye kufuga ni wafugaji wanahamahama kila asubuhi hawana uhakika wanafugaje mifugo yao watanenepa saa ngapi kwa kuwatembaza katika nchi nzima. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tungetengeneza utaratibu mzuri ule ambao nilitoa mchango wangu wakati nachangia kwenye bajeti kwamba zile *NARCO* wapewe hawa *free* tuwaondolee na ile kodi, wapewe hawa *free* wakaka kule, wakikaa kule ng'ombe wanatenepeshwa vizuri, watakwenda kuwapeleka kwenye michakato kwenye viwanda vizuri, na watapata bei nzuri kwasababu ng'ombe atakuwa na uzito unaostahili. Lakini hivi wanavyochunga kuanzia asubuhi wanazurula kutwa nzima nchi nzima ng'ombe huyo atakuwa saa ngapi atanenepa saa ngapi mpaka atoshe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Kibaha Vijiji kuna maeneo ya Gwata, Maeneo ya Dutumi maeneo ya Magindu wako wafugaji wengine wachache pale wanagombana kila siku na wakulima na wafugaji maeneo hayatoshi. Na nikumbushe hapa tutumie mfano mmoja wa uanzishwaji wa vijiji vya ujamaa, nchi yetu wakati inaingia kwenye uanzishwaji wa vijiji vya ujamaa Mwalimu alitaka Watanzania tusogee tukakae maeneo pamoja ili tuweze kuhudumiwa vizuri. Ni imani yangu kama Wizara ya Mifugo itatumia zile *NARCO* wakawaweka hawa wafugaji pamoja watawahudumia vizuri na mifugo itakuwa mizuri na itakavyokuwa mizuri ndivyo itakavyokwenda kwenye viwanda hivi vinavyochakata vikiwa na unene unaofaa na watakwenda kupata kilo za kutosha na wao watapata bei inayofanana na kile ambacho kinakusudiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nishauri tu Serikali iangalie upya tozo hii, iangalie vizuri kwasababu wasiwasi wangu umekaa katika mazingira ya kwamba hawa watu wa kati hawatapeleka mifugo hii kwenye vile viwanda vinavyochakata na watakataa kupeleka huko kwa sababu watatakiwa wakatwe hii tozo ya asilimia mbili na hii sio fedha ndogo ukipigia hesabu kwa mazingira wanayozalisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pale *Tan Choice* wananiambia kwa siku wanataka kuchinja ng'ombe wasiopungua 1,000. Mpaka leo hii wanachinja ng'ombe 80

tu, ng'ombe hawafikishwi pale wakati kiwanda kipo na kikubwa kina uwezo. Shida ni mazingira ya upatikanaji wa mifugo hiyo na hizo tozo zinaweza zikawa nyingi zikawa tatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, baada ya kusema haya, nishukuru na naunga mkono hoja lakini kwa kweli hii tozo naomba iangaliwe mara mbili, mara tatu. Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Naambiwa kuna wageni wengine ambao hatukupata fursa ya kuwatangaza. Kuna wageni wa Mheshimiwa Flatei Massay, Mbunge wa Mbulu Vijiji, ambao wapo 11 wanaongozwa na Mchungaji Tumaini Mao na Mwenyekiti wa Kijiji Elibariki. Karibuni sana wageni kutoka Mbulu Vijiji. (*Makofi*)

Wapo pia wageni wa Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, ambao ni watoto wake lakini pia yupo mdogo wake. Mdogo wake ndiyo anaongoza hawa wote anaitwa Justa Emmanuel. Watoto wake ni Victor Kaiza na Verona Kaiza na mtoto wa ndugu yake anaitwa Briana Kaiza. Karibuni sana. (*Makofi*)

Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau, atafuatiwa na Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo, Mheshimiwa Constantine John Kanyasu ajiandae.

MHE. EDWARD O. KISAU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Nimpongeze Waziri wa Fedha na Naibu wake na timu nzima kwa kuleta hotuba nzuri inayohusiana na *The Finance Bill*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianzie kwenye Mabadiliko ya Sheria ya Kodi, section 23 ya *Finance Bill* ambayo watu wengine walikuwa wanazungumzia hii kodi hii ambayo ni *two percent withheld* kwa mazao yanayotokana na kilimo, mifugo na uvuvi. Nawapongeza Kamati ya Bajeti ambayo wameichambua sana na hata wao wameona. Kama

alivyosema Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake nia sio kumtoza mkulima ama mfugaji au mvuvi lakini sasa sheria haiko *clear kum-protect* mtu huyo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu *amendments zime-define a resident cooperation*, pale anaponunua vitu kutoka kwa mtu anayeitwa a *resident person*. Sasa *a resident person is not defined*. Sasa isipoangaliwa vizuri inawezekana baadaye huyo *resident person* aka-*include* mkulima, mfugaji na mvuvi. Kwa hiyo, kwa jinsi mlivyo-*define* hiyo *resident cooperation* ni vizuri pia m-*define a resident person* huyu sasa ambaye anaauza kama mlivyo-*define* vizuri kwamba *resident cooperation* hai-*include SACCOs, AMCOS* na vitu vingine. Nahofia tusije tukajikuta kwamba yule ambaye tulitaka *kum-protect is not protected*. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naangalia hotuba ya Mheshimiwa Waziri hapa, kuna *paragraph* ambayo *is not clear* kwenye hizi *amendment* na nia yake ilikuwa ni nzuri sana. Kuondoa sharti lile linalomlazimisha mlipa kodi ambaye anataka ku-*object* ile *assessment* la kulazimishwa kulipa *one third* kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 13 wa hotuba yake. Sasa ukiangalia sasa Sheria ya Kodi, *section 51* ambayo ndio inaleta sharti hilo haipo kwenye *amendment*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni vizuri pengine muangalie kama nia ilikuwa ni kuondoa sharti lile kwa sababu nilieleza vizuri sana siku ile, ukasema ni kweli mtu anaweza aka-*inflate* ile *tax*. For example, one third of 30 billion is too much. Kwa hiyo, ni kweli kama sharti ilikuwa ni *ku-relax* hii, basi muangalie *section 51* kwa sababu ndiyo inayozungumzia masharti hayo na haiko kwenye *amendment*. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia pia kwenye Kamati na *Schedule of Amendment* iliyoletwa na Serikali, kulikuwa na wazo la kumfanya Mkaguzi wa Hesabu za Serikali ku-*audit* mashirika ambayo Serikali ina *more than 50 percent share* na inaonekana Kamati na Serikali wamekubaliana. Hata hivyo, ukiangalia ile *Finance Act definition* iliyoletwa

inatolewa kwa *public authority* imekuwa *extended Zaidi*, imekuwa *more broaden ku-include* vitu vingi sio *share* peke yake, kuna vitu vingi sana *vimeongezwa* pale ambavyo *actually ina-justify* sasa kwamba hata anaweza aka-*audit* yale ambayo hata kama Serikali haina 50 percent *share*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuna haja ya kufanya *re-alignment* kuangalia *exactly intention* ilikuwa ni nini. Kwa sababu unavyo-*broaden definition* ya *public authority* ku-*include* vitu vingine *beyond* ile 50 *share*, maana yake unakaribisha sasa *intention* ya *ku-audit* hata zile nyingine. Kuna Mheshimiwa Mbunge alisema hata pale tunapoweka dhamana kwa miradi hii ambayo tuna ubia na watu wengine *regardless* ya *share it is good iwe-audited* na *I think hii amendment* ilikuwa inajaribu ku-*cover more broadly* vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nyingine ambayo nilitaka kugusia kidogo ni *TARURA*. Kuna hili suala la *TARURA* ambapo tunawasifu sana na hata mlivyoweka kwenye *amendment* ya kifungu kile ni nzuri sana. *My own concern* ni moja, unajua tulishasema hivi tunahitaji fedha nyingi sasa ziende *TARURA*, kwa hiyo, hatulindi ile 100 peke yake mnayoongeza kwenye mafuta, tunataka pia ku-*revisit* ile *formula* ya *TANROADS* na *TARURA* ambayo imekuwa ni 30 percent na 70 percent ambayo tulisema *it is unfair*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Mbunge nilikuwa naongea naye akaniambia *in fact* kwa kuwa tuliwapa mzigo mkubwa sana *TANROADS* kwa sababu walikuwa na kazi ya kuunganisha mikoa mingi na hiyo kazi imepungua *actually*, imebaki tu sasa barabara ya Kiteto, Dodoma, Arusha, Tanga, Manyara na Kigoma na sehemu zingine chache sana. Kwa hiyo, *it is high time* na kwa kuwa llani yetu inazungumza kwamba tureje *formula* ile ya *TANROADS* na *TARURA*, hizi *amendment* tunavyoenda kuzifanya ni vizuri Mawaziri wale wakaja pia na *formula* sasa, sio tu ku-*protect* hii *one hundred* ambayo tunaweka kwenye mafuta lakini kuangalia sasa ile *formula* ya Mfuko wa *TARURA* na *TANROADS* ili Mfuko huu uwe na fedha nyingi zaidi ili barabara za vijiji za ziendelee kuwa

nyingi zaidi. Kwa hiyo, ni vizuri muangalie kwenye *amendment* hiyo ili fedha ziweze kupatikana zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho nimekiona kuna *amendment* ambayo nia *I think* ilikuwa ni njema, pale mnaposema mnataka ku-*defer 12 months* kabla ya ku-*impose* ile *restriction* ya yale makampuni kuwa na *saver*. *Section 64* mnasema kwamba *amendment* inayohusiana na *primary saver* na *sub-section (8)* na *(10)* zinakuwa *deferred* zianze kufanya kazi *12 months later*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, huko mbele tena *section 71* mnataka kuleta *offence* kwa mtu ambaye ata-*fail* / *ku-maintain* ile *primary saver*. Sasa kama una-*defer* hizi *sub-sections* tatu maana yake ni kwamba hata hii *section 71(m)* ambayo ina-*impose offence* kwa yule ambaye ata-*fail* kuweka ile *primary data saver* lazima pia iwe *deferred*. Otherwise mtaleta *confusion* mna-*defer section* zinazo-*put obligation* kwa mtu kuwa na hiyo *primary data* lakini yule ambaye hatakuwa nayo unataka kum-*punish even before 12 months* ambayo ulitaka ku-*defer*. *I think it is a drafting issue*, ni *issue* tu ya ku-*realign* ili ikae vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache sana, nakubaliana na *amendments* hizi, *I think* nia ni njema sana na imekubaliana na mawazo mengi sana ya Wabunge. Nakushukuru sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo, atafuatiwa na Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Mheshimiwa Almas Athuman Maige, ajiandae.

MHE. VEDASTUS M. MATHAYO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Muswada huu ulio mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusema kweli na mimi naungana na wenzangu wengi kukushukuru sana Waziri wa Fedha, ndugu yangu Mheshimiwa Mwigulu kwa bajeti yako nzuri hasa hasa ulipokuja kumalizia wakati una-*windup*,

maana watu wakiona mabadiliko yoyote yale ni utaratibu wa kawaida kwamba lazima *wa-complain*, kama pale walipoona umeweka Sh.100/= kwenye mafuta tafsiri rahisi ikaonekana kwamba basi kila kitapanda.

Sasa ulipokuja kumalizia, nadhani wewe mwenyewe uliweza kuona kwamba kila mmoja aliweza kukupongeza. Kwa utaratibu unaoenda nao ni imani yangu kwamba karibu watu wote ni rahisi sana kuwagusa. Kwa hiyo, hongera sana kwa hilo Mheshimiwa Waziri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi nichukue nafasi hii kwanza kuipongeza Serikali, wakati fulani hivi Wabunge mtaona tunalamikalalamika kwamba tunapotoa mawazo yetu Serikali wakati mwengine inayapuuza. Ni ukweli usiopingika kwamba kila Mbunge anapokuwa anatoa mawazo huwa anaamini kwamba hayo mawazo yake ni sahihi. Kwa hiyo, wakati mwengine mna kazi ngumu ya kuona namna ya kuya-*accommodate* yote. Mimi ninao ushahidi thabiti ambao umeendelea kuonyesha kwamba mambo mengi ambayo tunayazungumza basi huwa mnayachukua na huwa mnayafanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka nilipoingia katika Bunge hili mwaka 2005 kwa mara ya kwanza, kati ya hoja ambayo niliishupalia sana ilikuwa ni hoja ya hawa ndugu zetu wa bodaboda. Serikali ilinisikiliza na hatimaye ikawaweka rasmi, ikawatambua na wakaendelea kufanya kazi kama watu wengine au kama wasafirishaji wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nakumbuka tena katika mchango wangu niliweza kusema kwamba hawa bodaboda wanalipa faini ya shilingi 30,000 anapofanya kosa lakini huyo bodaboda anabeba abiria mmoja, dereva anayebeba abiria 60 au anayeendesha gari kubwa naye bado analipa faini ya shilingi 30,000. Mheshimiwa Waziri nikupongeze sana na nikuambie tu kwamba bodaboda wengi wamefurahi kuona kwamba tumeweza kuwapunguzia adhabu kutoka shilingi 30,000 mpaka shilingi 10,000. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba kila jambo lina pande mbili; lina faida na hasara. Niliisikia humu baadhi ya *concernza* Waheshimiwa Wabunge wakisema kwamba kile kitendo cha kuwapunguzia adhabu sasa inawezekana kikasababisha ajali zikawa nyingi, kwa hiyo, hilo nalo linawezekana likawa tatizo.

Sambamba na hilo nilikuwa na ushauri, hivi tunadhani ni kwa nini bodaboda wanababisha ajali? Pamoja na sababu zingine lakini sababu moja kubwa ni kwamba bodaboda wengi wanapoendesha zile bodaboda hawana leseni na kwa sababu hawana leseni akiwa amepakia abiria akimuona tu *traffic* maana yake ni kwamba yeye sasa hachagui mahali pa kwenda, mahali popote anaruka matokeo yake abiria wanaanguka lakini vilevile ni pamoja na kusababisha hizo ajali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuijulize kama kweli lengo letu tunahitaji kuwasaidia hawa watu wa hali ya chini ili na wao waweze kupata maisha mazuri, maana na wao nao wana mahitaji kama ya wale watu wenye kipato cha kati na cha juu, ana watoto anataka waende hospitali, anataka waende shule, ana mke anataka amuhudumie.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu inayochangia hao bodaboda kukosa leseni ni kwa sababu ya gharama kubwa ya leseni. Gharama ya ye yole yule anayetaka leseni hata wa bodaboda sio chini ya shilingi 300,000 maana lazima aende kujifunza kwanza aidha ni *VETA* au mahali popote ataacha fedha hapo, akitoka hapo ndio aende kwenye kulipia gharama zenyewe za leseni kule *TRA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kutokana na hali hiyo unamkuta yule bodaboda analipa sio chini ya shilingi 300,000 lakini na yule anayetaka leseni ya kuendesha gari kubwa naye gharama zake ni hizohizo shilingi 300,000, ukiangalia hapa kuna shida. Kwa hiyo, kwa sababu hawana uwezo wa kulipa marejesho na kulipa hizi shilingi 300,000 matokeo yake anaamua kuendesha bodaboda pasipokuwa na leseni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba ni vizuri hilo Waziri wa Mambo ya Ndani akaliangalia na mkaona namna ya kutoa maelekezo. Hawa bodaboda wawe na utaratibu maalum ikiwezekana kwanza wafundishwe kwa muda mfupi lakini yatolewe mafunzo yao kwa Pamoja. Hili mimi nalisema kwa sababu nilishalifanya, nilishakaa na watu wa *VETA* na watu wa *Red Cross* wakakubali kudhamini pamoja na Ofisi ya *RTO* tukatoa mafunzo maalum kwa vijana wasiopungua 60 walipata leseni siku moja kwa gharama nafuu. Sasa hili likiwa kwa nchi nzima na tukaweka utaratibu mzuri wa namna hiyo basi unaweza ukasaidia zaidi katika kupunguza ajali kuliko hali ilivyo hivi sasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo Mheshimiwa Waziri kuna jambo dogo ambalo liko kwenye ofisi yako. Kwenye ofisi yako kwa maana ya *TRA* mmeajiri vijana wasiopungua 600 mmewapa ile ajira ya muda, ile ya kujitolea na mnawapa ujira mdogo sana kwa mwezi na wale vijana wanafanya kazi nzuri sana lakini shida inakuja wapi? Inapofika wakati mnapotaka kuajiri hamuwapi wale vijana kipaumbele. Mnapotaka kuajiri mnatoa tangazo kwa kijana ye yote yaani ambaye ameshakaa pale na ambaye hajakaa pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta kwamba kijana amekaa pale miaka mitatu, mnamlipa ujira kidogo halafu inapofika wakati wa kuajiri wakati mwengine huyo mnamuacha na wakati tayari ameshapata uzoefu. Nadhani hili si jambo zuri sana ni vizuri mkawapa wale kipaumbele kwa sababu mmeshawa-*retain* pale for three years na wamepata uzoefu na wanaweza kuwasaidia vizuri zaidi kuliko kuja kuchukua vijana wengine kutoka nje na kuwaajiri halafu wale mnawaacha. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani hili lingine ni la huko mbele tunakoenda kwamba ni vizuri tukatambua kwamba leo katika nchi hii kama kuna mahali ambapo tuna shida, tunao vijana wengi wanaomaliza vyuo, sekondari au darasa la saba wengi wao hawana ajira. Ni lazima tuangalie mkakati

wa kutumia kwamba hivi hili wimbi tunaweza kulipunguza kwa namna gani. Kwa hiyo, nadhani hilo nalo ni *assignment* ambayo wewe kwa nafasi yako una kila aina ya sababu ya kulifanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, atafuatiwa na Mheshimiwa Almas Athuman Maige, Mheshimiwa Yahya Ally Mhata ajiandae.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nami naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri lakini na Serikali kwa ujumla, kwa kuchukua sehemu kubwa sana ya maoni ambayo tulitoa, lakini na kufanya kazi malalamiko ambayo yamekuwepo kwa muda mrefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nilitaka niweke maelezo machache kwa alichosema Mheshimiwa Mathayo, wengi tunasema pikipiki inabeba mtu mmoja, lakini ukweli ni kwamba pikipiki ninazokutana nazo mimi barabarani zinabeba watu wanne mpaka watano. Sasa inawezekana kishawishi hiki cha kupunguza faini kisiposimamiwa vizuri tutatengeneza wodi 10 za majeruhi kule Bugando na kule Muhibili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimewahi kushuhudia pikipiki imeua watu watano. Iliingia kwenye trekta ikaua dereva wa pikipiki na abiria wake wanne. Sasa hapa tunazungumzia mtu mmoja, lakini nadhani kuna haja ya kusimamia vizuri sheria hapa ili kuwafanya madereva wa pikipiki kufaidika na pungozo la faini lakini kuhestimu sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, alitusikia kwenye uvuvi, lakini maelezo yake kwenye hotuba yake naona kama hayakueleweka vizuri. Amesema na ninaomba nimnukuu, alikuwa

amezungumzia kutoza kodi ya zuio kwa kiwango cha 2% kwenye malipo yanayohusisha mauzo ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi yanapouzwa kwenye makampuni ya mashirika yanayojihusisha na usindikaji wa mauzo ya mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, pendekezo hili halitahusisha wakulima akawaacha tena wavuvi hapa, hawapo kabisa; pendekezo hili halitawahusisha wakulima wadogo na wale wanaouza mazao yao kwenye Masoko ya Msingi, *AMCOS* na Vyama vya Ushirika. Yaani hapa hakuzungumza mvuvi kabisa, amemsahau. Huku juu amezungumza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, madhara yake ni kwamba mvuvi anapopeleka samaki kiwandani; ukiona samaki ziko kiwandani, pale katikati unaweza ukafikiri kuna mfanyabiashara au kuna Chama cha Ushirika. Hakuna Chama cha Ushirika cha Wavuvi, hakipo. Wavuvi wanaokusanya tani tano ni wavuvi wanaokwenda ziwani na kuleta kilo kumi kumi. Baadaye wanazikusanya na kuzipeleka kiwandani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa maelezo yako hapa yasipokuwa wazi vizuri, yatamfanya huyo aliyepeleka kiwandani kutafsiriwa kama *middlemen* au kutafsiriwa kama mfanyabiashara mkubwa na kukatwa 2%. Mheshimiwa Waziri naomba uliweke vizuri kama uliviyokusudia huku juu ili liwataje wavuvi hawa tunaowazungumzia kwa sababu ni wale wale tunaowalenga ambao wanakusudiwa kuondoa tozo hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vinginevyo nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuendelea kwenye suala la *cold rooms* kwa maua. Nirudie kusema, kwamba Dodoma na miji mingine mingi tunakula samaki waliooza. Kwa sababu samaki unayemtoa kwa mvuvi mwenzangu hapa Mheshimiwa *Eng. Stella Manyanya* kuwaleta Dodoma wakiwa kwenye *lorry* ambalo haliko *refrigerated*, wanafika wameoza. Samaki unaowatoa Mwanza wakiwa *chilled* kwenye barafu, halafu baadaye wanapelekwa kugandishwa, hawagandi kwanza,

hawafikii *freezing point* ambayo ni *recommended*, wanakuja hivyo hapa na wengi wanafika wameoza. Maana yake ni nini? Hatuna *refrigerated container*wala *refrigerated trucks* ambazo zingeweza kusaidia kum-*Maintain quality*ya samaki na kupunguza *cost harvest loss.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nakubaliana na hoja hii kwenye maua lakini naomba kumsisitiza Mheshimiwa Waziri atuombee msamaha kwenye *refrigerated container* ili tuweze kusaidia kwenye nyama na samaki. Hivi leo tunavyozungumza, ukikutana na nyama inasafirishwa kutoka machinjioni kwenda kwenye *butcherutafikiri* wanapelekewa labda mbwa; kwa sababu ni magari ambayo hayana *quality* na wala hayakuandaliwa vizuri. Ni kwa sababu ya sheria hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Sheria ya VAT 148 Sehemu ya Tisa Mheshimiwa Waziri amezungumzia kuhusu viwanja; misamaha ya nyasi. Amezungumza tu kuhusu Majiji na Mapispaa; mwanzo alikuwa kwenye Majiji sasa kaongeza Manispaa. Katika nchi hii tuna mikoa minne ambayo bado ni Halmashauri za Miji. Mkoa wa Geita ni Halmashauri ya Mji; Mkoa wa Katavi ni Mji, Mkoa wa Njombe sijui na wapi; hii ni mikoa ambayo umeiondoa kwenye misamaha yako, umepeleka kwenye Manispaa na kwenye Majiji. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri kwenye Mikoa hii Makao Makuu ya Mikoa uongeze kwenye msamaha wako wa kodi wa Nyasi Bandia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambao nataka kusema hapa, tulisema tunataka kuongeza uwezo wa Halmashauri kukopa. Zipo Halmashauri 34 tu ambazo zimefaidika na mikopo ya fedha kutoka Serikalini. Hizi Halmashauri 34, nyngine zimekopa mara nne, mara tano na mostly ni Dodoma na Dar es Salaam. Halmashauri zote Tanzania hazijafikia uwezo wa kujitegemea. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri, masharti yaliyokuwa yamewekwa ni kama yalikuwa yanapunguza uwezo wa wakopaji badala ya kusaidia wakopaji kuongezeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri zote zilizoandika andiko zimeonekana maandiko yake hayana sifa kwa sababu walioandika hawana sifa, lakini waliota maelekezo ya kuandika ni Serikali na walioandika ni Serikali. Sasa mimi nimekuwa nikipata taabu, ambao hawana sifa ni waliota mafunzo ya uandikaji wa andiko au ni walioenda kuandika na kusahihisha andiko kwenda kwenye kukopeshwa? Kwa sababu fedha zipo kwa mujibu wa Serikali, lakini wakopaji hakuna na Halmashauri ni masikini. Kwa miaka mitano zimekopeshwa Halmashauri chini ya 30; na waliokopeshwa wanalazimishwa kubuni miradi ambayo Halmashauri hazina vipaumbele. Kwa mfano, usishangae kuona Halmashauri zote zinakopa kujenga stendi na masoko, ndiyo miradi ambayo inalipa kwenye Halmashauri husika. Ninyi mkija huku mnasema hapana, *this is copy and paste*. Ni *copy and paste* kwa sababu kule kwangu Geita stendi ndiyo mradi ambao unalipa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri, aidha Kamati hii ambayo inasimamia na kuchambua ipeleke mafunzo sahihi kwa wakopaji au irekebishe masharti ya kukopa isionekane kama masharti yametengenezwa kupunguza wakopaji. Kwa sababu unaweza kutengeneza masharti ya kupunguza wakopaji na utashindwa kuisaidia Serikali kuongeza mapato. Jambo hili ni muhimu sana kwa sababu tunazungumzia Halmashauri ambazo nydingi hapa sasa umebeba mzigo wa kuzisaidia, lakini kuna mafungu ya fedha Serikali imeandaa kwa ajili ya kusaidia Halmashari kuweza kuijendesha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuongeza fedha za mikopo hasa ya Elimu ya Juu. Zitaongezwa pale shilingi bilioni 70, lakini kilio ambacho tumekuwa nacho ni *formula* ile ya utoaji wa mikopo. Ile means test bado haiwezi kuwa very transparent. Mimi nina watoto hapa zaidi ya watatu ambao ni wapiga kura wangu; ni yatima na wemekosa mikopo. Yaani unamwona mtoto mpaka shule ameacha, chuo ameacha, lakini ana sifa za kukopeshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tumeongeza shilingi bilioni 70, ninataka kutoa ushauri; wachambuzi wale wanaokopeshwa wanasema wale wanaojaza fomu za maadili hawakopeshwani. Unajua wanaojaza Fomu za Maadili ni pamoja na Madiwani. Diwani analipwa shilingi 350,000/=, angekusanya posho zake zote, hazifiki shilingi 600,000/=, lakini ni sehemu watu ambaye mtoto wake akiandika kuomba kukopeshwa, siyo sehemu ya wanaokopeshwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kutoa ushauri, kwa kuwa Serikali imeongeza fedha; na fedha hii ni ya mkopo, kila mtoto wa Kitanzania anayeomba kukopa maadam ni mkopo, apewe mkopo. Kama tatizo ni fedha, tuje na kiwango ambacho ni *minimal rate*. Kwa mfano, unaweza ukasema *at minimal/tutakupa 30%* kwa sababu wewe baba yako ana uwezo wa kulipa; lakini *as long* nami mzazi nimesema mkopeshe huyu mtoto, ni kwa sababu niimeangalia *may be* nina watoto wengi wanaosoma, uwezo wa kuwasomesha sina na Serikali inakopeshwa na mtoto atalipa, aweze kukopeshwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *as it is now, as long as wewe* ni Mbunge, haijulikani una watu wangapi unasomesha, watoto wako hawakopesheki; wewe ni Diwani, watoto wako hawakopesheki; wewe ni Mkuu wa Idara, watoto wako hawakopesheki. Mheshimiwa haka bado kanatengeneza ka aina fulani ka ubaguzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuondoa *SDL* kwenye hospitali, kwa watumishi wa Hospitali ambao kimsingi wanafanya kazi ya Serikali.

Sasa tuendelee taratibu, hata shule binafsi zinazofundisha watoto wetu zinafanya kazi ya Serikali. Watoto 20,000 walioko kwenye shule binafsi wakiondoka wakaenda kwenye shule za Serikali mtatengeneza madawati, mtajenga madarasa, mtaongeza walimu, mtanunua chaki, mtaongeza kila kitu kule ndani. Sasa kama umeweza kufanya huku, tulitazame hilo ili tuweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, nimekumbushwa hapa mbele, hoja iliyopo mbele yetu ni Muswada wa Sheria ya Fedha. Japokuwa vina uhusiano wa karibu kabisa na Bajeti Kuu, lakini tusichanganye mambo mawili, kwa sababu Waziri sasa hivi anaangalia vifungu pale. Ukiwa unachangia, anaangalia ni kifungu gani ambacho unapendekeza kirekebishwe au kuna jambo kwenye kifungu fulani hakijaeleweka vizuri. Sasa tukichangia Bajeti Kuu, Muswada huu utapita kama ulivyoletwa kwa sababu michango ya Waheshimiwa Wabunge itakuwa haipo kwenye huo Muswada. Kwa hiyo, hoja iliyopo mbele yetu ni Muswada, hivyo, tujitahidi kuweka michango yetu kwa namna hiyo.

Mheshimiwa Athuman Almas Maige, atafuatiwa na Mheshimiwa Yahya Ally Mhata na Mheshimiwa Kasalali Mageni ajiandae.

MHE. ATHUMAN A. MAIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana nami kuniruhusu nichangie Muswada huu wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2021/2022. Muswada huu umelenga kukusanya fedha ambazo zitatumika katika Mpango wa Bajeti ambayo tumeipitisha hapa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Orodha ya Sheria ambazo zitarekebishwa ipo katika ukurasa wa pili na wa tatu wa Muswada wenyewe huu. Naomba nijikite katika maeneo yafuatayo; nianze kwanza kuishukuru sana Serikali. Kwa mara ya kwanza Serikali imefanya jambo kubwa sana la kusaidia kutuletea bajeti ambayo itasaidia wananchi wa chini kabisa wa nchi yetu na kila mwananchi atafaidi kutokana na bajeti hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nijikite kwenye mambo yafuatayo; kwanza Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis Stadi

Sura ya 82. Idadi ya chini kabisa ya wafanyakazi watakaolipiwa *SDL* kutoka wanenewa kwanza mpaka 10. Hii imetusaidia sana, lakini *SDL* tunayolipa hapa nchini ni kubwa sana, asilimia nne. Katika nchi zote za *East Africa*; hizi za Afrika Mashariki na *SADC*, ya juu kabisa ni 2%. Tunaomba kwenye bajeti ijayo, mwaka unaofuata, basi *SDL* tena iteremke kidogo baada ya kuongeza maeneo fulani ya kodi. Nami nashauri Serikali ijkite kwenye kupanua wigo wa kodi na eneo moja ambalo lina kodi kubwa ambayo haijulikani sana sana ni sekta ya ulinzi binafsi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri Serikali hebu ilete Sheria ya Sekta ya Ulinzi hapa Bungeni tuweze kuyatambua Makampuni yapo mangapi; yana wafanyakazi wangapi? Watalipwa *SDL* kubwa na kodi itapatikana badala ya kung'ang'ani kiwango kikubwa cha *SDL* kipungue kutokana na uwingi wa watu watakaolipa *SDL*. Hilo la kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Muswada huu utarekebisha Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta Sura ya 220 ili kupata fedha za *TARURA*. Suala hili ni zuri sana. Tumeweka kiwango kidogo sana, shilingi 100/= kwa aina yote ya mafuta kwa lita, lakini fedha hizi zitakuwa nyingi sana. Wabunge humu tunatumia lita ngapi kwa siku? Wananchi wa Tanzania nzima wanatumia lita ngapi kwa siku?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sio mtaalam wa mafuta, lakini nafiriki nikifumba macho naota mahela mengi yatakayopatikana. Sitaki tuje tuone aibu hapa. Waziri wa Fedha awe na fedha nyingi ambazo hajui pa kuzipeleka. Tuzipeleke kwenye Mfuko wa *TARURA* ili tuone kweli barabara zinajengwa kutokana na mfuko huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Muswada wake amesema kutakuwa na Mfuko Maalum wa *TARURA* ambapo fedha zitakwenda siyo kwenye *Central Account* halafu zianze kuchukuliwa moja moja. Jambo hili likitekelezwa, wananchi hawatakuwa na kilio cha kupandishiwa nauli kidogo, wataona barabara hii haikuwepo imejengwa, pale palikuwa hakuna barabara, pamejengwa; itasaidia kuzima kelele za

lawama kwa Waziri kwa bajeti hii iliyoleta fedha za *TARURA*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Nane inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Kodi Na. 332; Sehemu ya Nne, kupunguza *Payee as You Earn*. Jambo hili watu ambaao sio waajiri kama vile halina mhemko, halina *impact*. Kwa kweli limetusaidia sana na wafanyakazi wenyewe pia kutoka asilimia 11 tuliyokuwa nayo wakati tunaanza Bunge hili mwaka 2015 mpaka 8%, ni fedha nydingi sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukichukua tu *Wage Bill*, yaani gharama ya mishahara kwa mwezi kwa Serikali, shilingi bilioni 600, hebu toa 1% ile, ni fedha nydingi sana. Hata sekta binafsi inaa jiri wafanyakazi wengi sana. Kwa hiyo, asilimia hii ndogo imetupa nafuu na Serikali tunalpongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sehemu ya Tisa; marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Majengo. Hapa kuna utata. Maelezo ya Mheshimiwa Waziri juzi, Sura 289, jana yamekuja maswali sana. Wanasema sasa kodi italipwa kwenye Luku. Ghorofa 28 zipo na watu wa kazi kwenye sehemu mbalimbali ya jengo hilo kuna Luku. Sasa hivi tunalipa kodi hii mara moja kwa mwaka, sisi wenyewe majengo. Tunalipa kodi mara moja kwa mwaka ya jengo, mwezi Julai.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sijui Mheshimiwa Waziri alikuwa na maana gani kwamba kila tunaponunua umeme tutalipa kodi, itakuwa kila unaponunua umeme unalipa kodi, hakutoa maelezo ya kutosha. Je, hao wananchi au watu wanaokaa kwenye jengo la fulani ambaao wapo 300 kwenye Luku 100; watakatwa fedha ambayo watampelekea tena Ankara huyu mwenye jengo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri hakutoa maelezo, atueleze hilo, kwamba hawa wapangaji wangu mimi wataniletea hiyo *bill* waliyokatwa niwarudishie wao? Kwa sababu ninayetaka kulipa kodi ni mimi mwenye jengo. Haya ni masuala ambayo hayakueleweka vizuri. Ni jambo

zuri sana kwamba kodi kweli italipwa, lakini kiwango kikubwa cha majengo hapa pia hayatumii umeme; ni asilimia ndogo sana umeme upo katika majengo ya mjini, lakini kuna majengo mazuri ukipita barabarani hapa Kibaigwa, sijui wapi, ukienda Chalinze kuna majengo mazuri sana yanatakiwa yalipe kodi. Mengine hayana umeme na mengine yana umeme, itakuwa tunapata taabu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maoni yangu nafikiri kwamba, huu uchukuaji wa kodi ni mzuri sana, lakini yanatakiwa maelezo zaidi, nani atalipa mwishoni? Mwenye jengo au hao wenye Luku wamekuwa wachangiaji wa kodi ya jengo?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na huo ndiyo mchango wangu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, atafuatiwa na Mheshimiwa Kasalali Mageni na Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi ajiandae.

MHE. YAHYA A. MHATA: Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba nichukue nafasi hii kuchangia huu Muswada wa ukusanyaji wa fedha au *Finance Bill* ambao uliwasilishwa na Mheshimiwa Waziri. Muswada huu ni mzuri na una lengo la kuisaidia Serikali kuweza kukusanya fedha ili yale ambayo tulikubaliana yaweze kutendeka. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali, nampongeza sana Waziri mwenye dhamana na Wizara hii kwa kazi nzuri aliyoifanya kwenye bajeti ya mwaka huu na huu Muswada aliotuletea. Nina uhakika leo hii narudi ndani ya Jimbo langu nikiwa na uhakika wa vyanzo zaidi ya vitano vyenye fedha, zaidi ya shilingi bilioni tatu katika Jimbo langu. Nina uhakika wa kupata shilingi milioni 500, jambo ambalo halijawahi kutokea katika nchi hii. Narudi mwezi huu jimboni kwangu nikiwa nina uhakika wa bilioni 1; narudi nikiwa na

uhakika wa shilingi milioni 600 kwa ajili ya ujenzi wa shule; na ninarudi ndani ya jimbo langu nikiwa na uhakika wa maboma 10 kwenda kuyatengeneza. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, nina uhakika wa mradi wangu wa maji wa kutoka Mto Ruvuma kuja Mangaka utatekelezwa. Kwa kweli nampongeza sana sana sana Mheshimiwa Waziri kwa ubunifu mkubwa aliokuja nao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali, sasa tunarudi majimboni sisi Waheshimiwa Wabunge, mtuletee fedha hizi haraka. Huu Muswada tuupitishe ndugu zangu ili mwezi huu Julai na Agosti ambapo tutabaki majimboni, tuweze kusimamia fedha hizi zikafanye kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jana kulikuwa na *issue* ya *transfer price*; labda naomba nichukue nafasi hii kuwaeleze ndugu zangu *transfer price* ni nini na jinsi gani inatumika kwenye kuiibia Serikali. *Transfer price* ili iweze kufanyika lazima kuwe na Kampuni mama ambayo kwa lugha ya kigeni *parent company* na kuwe na *subsidiary company*. Sasa hii kampuni mama iponje ya nchi; hii kampuni nyingine *subsidiary* inakuja kwenye nchi yetu. Ndio inapokuja kufanyika *transfer price* na wenzetu Wahasibu walishaligundua hili, ipo *standard* kabisa *International Financial Reporting Standard (FRX) kama sikosei 12*, inayozungumzia *transfer price*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ili wizi huu ufanyike hawa wanatumia njia mbili, ile kampuni mama ambayo iko kule labda nchi yoyote tuseme nchi "A", inakuja kufungua mradi hapa labda wa uchimbaji wa madini, wizi wake unafanyika katika maeneo mawili. Moja, wana-over *invoice*, *ku-over invoice services* huku, ile kampuni mama imekuja kufungua machimbo ya madini kwetu, wale wanapotaka kutoa service katika ile kampuni yao ya huku, wanaichaji bili kubwa, wakiichaji bili kubwa wanapunguza kiwango cha kodi ambacho hii kampuni ambayo imefunguliwa hapa iweze kuilipa Serikali. Hiyo ni sehemu ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili kunakuwa na *factitious payment*, malipo hewa hewa, wanajifanya hii kampuni ya hapa inailipa ile kampuni mama kule, tumelipa hiki *Board of Director*, sijui tumelipa nini, anatumwa mtu kuja kutembelea hii kampuni analipwa ili kusafirisha fedha kule. Kwa hiyo ipo *financial reporting standard*, ambayo inasaidia kugundua mambo haya, wenzetu *ma-auditors* wakishaligundua hili.

Kwa hiyo inatakiwa kampuni hii inapofunga vitabu vyake i-*disclose* kama sisi ni *subsidiaries company*, kampuni mama ipo nchi Fulani. Asipofanya hivyo *Auditor* anakuwa na *two option*, moja anarudisha malipo yote yaliyofanyika kwenye ile kampuni mama kwamba sio halali, kwa hiyo yanatozwa kodi. Hata hivyo, kama amefanya inamlazimu sasa *Auditor* aangalie kwamba malipo haya yana uhali ali kiasigani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naishauri Serikali na naiunga mkono sana kama Mheshimiwa Mwigulu alivyosema, lazima tu-*press signal*, kwamba signal hii kwamba tunajua huu mchezo. Pili, wataalam wetu watambue kwamba sisi tunafahamu. Kwa hiyo mimi naomba ndugu zangu hii *transfer price* tuiachie Serikali na ile *proposal/yao*, ili hawa wafadhili waweze kuja, pia tutakuwa na uwezo wa kuwabana. Watakaokuja kufungua makampuni hapa tutakuwa na uwezo wa kuwabana kama tunafahamu na hata wataalam wetu watambue kwamba tunajua kuna mchezo wa *transfer price*. Hilo la pili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, Mheshimiwa Waziri alizungumzia masuala ya *property tax* na jinsi gani inatakavyokusanya. Naunga mkono kwamba ile asilimia 15 yote ipelekwe TAMISEMI na ikishapelekwa TAMISEMI ndipo pale watakapoanza kuzigawanya kwenye hal mashauri zetu. Mpango huu ni mzuri sana kwa sababu kuna baadhi ya miji ina *property* nydingi na kuna baadhi ya miji haina *property* za kuchaji hii *property tax*. Kwa hiyo, wazo la kukusanya na kupeleka TAMISEMI, halafu TAMISEMI wakatugawia kulingana na mazingira yetu, naliunga mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisisitize mifumo. Hivi karibuni tumegundua matatizo makubwa sana ya mifumo yetu, mifumo mingi imeingiliwa. Sasa kwa kuwa tunaingia katika utaratibu huu kuanzia mwezi ujao, naiomba Wizara iangalie mifumo hii iwe inasomeka. Leo TAMISEMI wana mifumo yao ya ukusanyaji wa mapato, Hazina wana mifumo yao ya ukusanyaji wa mapato na Bandarini wana mifumo yao ya ukusanyaji wa mapato. Sasa naiomba Wizara iisimamie mifumo hii iwe ni ya aina moja na isomeke, vinginevyo kutakuwa na athari ya kuleta hujuma katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja mia kwa mia ili mapato haya yatumike, yaweze kutuletea maendeleo katika Wilaya zetu. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Kasalali Mageni atafuatiwa na Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi na Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa ajiandae.

MHE. KASALALI E. MAGENI: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa nafasi hii. Kabla sijaenda kwa undani zaidi nimshukuru Mwenyezi mungu kwa uhai na uzima. Pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha na wasaidizi wake kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya, kuanzia kwenye bajeti kuu walipotuwasilishia ilikuwa nzuri, ina mwelekeo wakutatua hoja na shida za Watanzania na kwenye hii Sheria ya Fedha pia imejielekeza katika kutengeneza mazingira ya kukusanya pesa kwa ajili ya kuwaletea maendeleo Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia hii sheria katika vifungu vingi na maelezo mengi na mabadiliko mengi, mabadiliko yaliyofanyika ni mabadiliko rafiki kwa maendeleo yetu na hoja ambazo zilikuwa zinatolewa na Wabunge tangu tuanze kujadili bajeti, tangu Bunge la Bajeti likae mambo mengi yamejibowi hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka njielekeze kwenye jambo moja, kwa hiyo nitachangia mahususi kwenye hii Sura ya 220, vifungu nya 46 na 47. Hapa kuna hii Sheria ya Barabara na *Fuel Toll*, ambayo inazungumza kuhusu pesa Sh.363 ambazo zinakusanya kwenye kila lita ya mafuta. Katika hizi pesa Sh.100 ambayo imeongezwa inakwenda moja kwa moja *TARURA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kushauri hapa, kwanza niishukuru Serikali kwa *kui-ring fence* hii Sh.100 kwamba hii moja kwa moja inakwenda *TARURA*, inamaana inabakia shilingi 263.09. Sasa hii shilingi 263 iliyobaki, kabla ilikuwa inakusanya, kabla ya kuongezwa hii Sh.100, asilimia 30 ya hii pesa ilikuwa inakwenda *TARURA*, inaingia kwenye Mfuko wa Barabara inakwenda *TARURA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mazingira ambayo nayaona hii shilingi 78 ambayo ni asilimia 30 ya hii shilingi 263, tusipoiwekea utaratibu mzuri, tunaweza tukajikua tunatumia hii shilingi 100, na hii shilingi 78 ambayo tumeiwacha kwenye ule utaratibu wa asilimia 30 ambayo sheria katika kipengele "A" ambacho tumekirekebisha, imeeleza kwamba Waziri kwa kushauriana na Waziri wa TAMISEMI wataamua namna ya kutumia hii Sh.263, sisi tunasema ni 30 kwa 70, baina ya *TANROADS*na *TARURA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nina pendekezo, kwamba hii asilimia 30 na yenyewe ambayo ni Sh.78, tuijumlishe na Sh.100, ziwe Sh.178, *tuzi-ring fence*, tuzipeleke moja kwa moja kwenye Mfuko wa *TARURA*.

Kwa hiyo napendekeza badala ya kupeleka kwenye Mfuko wa Barabara, kama nafasi inaruhusu na mazingira yanaruhusu, tupate Mfuko wa Barabara *Vijiji*. Mfuko huu uwe unapelekewa hii pesa moja kwa moja, ili kuepuka matatizo yaliyokuwepo awali. Kwa sababu awali tulikuwa tunapanga bajeti za *TARURA* na hii ipo, lakini mara nyingi bajeti za *TARURA* zilikuwa hazifikii malengo. Mara nyingi pia tulikuwa tunaacha uwazi wa hii asilimia 30, hii Sh.78, tunakuwa hatuna uhakika kwa asilimia zote kama yote imekwenda *TARURA*. Sasa ili

tuwe na uhakika kwamba tumeongeza Sh.100, tumeongeza na Sh.78, hizi Sh.178.09 zote zinaenda kwenye Mfuko wa Barabara Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala la *TARURA* tulilipiga kelele sana kwa sababu ni swala ambalo linatoka kwa wananchi wa vijijini moja kwa moja, barabara za vijijini hazipitiki na bajeti hii ya *TARURA* ilikuwa haikidhi mahitaji. Sasa tumeongeza Sh.100 na hii 78 zote tuzipeleke kule. Mheshimiwa Waziri hizi pesa za *TARURA* tunashauri sasa ufile wakati tuwe tunazipeleka kwa asilimia mia moja. Leo ninavyozungumza kwenye Jimbo la Sumve, tumepokea asilimia 91, asilimia ile iliyobaki kuna barabara muhimu sana zimeshindwa kumaliziwa ambazo zilikuwa kwenye bajeti. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Barabara ya kutoka Nyambui kwenda Manda na Barabara ya kutoka Mwitambu kwenda Kiminza zilikuwa kwenye pesa milioni zaidi ya 77 zimebak. Hili ni chomekeo kuonyesha ni kiasi gani fedha za *TARURA*, zisipowekewa utaratibu tutakuwa hatutekelezi yale matakwa ya kupeleka barabara vijijini zikapitike. Sasa tunaishukuru sana Serikali kwenye upande wa *TARURA*, kwa kweli mwaka huu mmetupa raha, kama ambavyo wengi wamesema milioni 500 tumeshapewa, tumeshaahidiwa bilioni moja huko mbele, mambo ni mazuri, lakini sasa kwenye hili naomba tuweke sheria na utaratibu ambao utaifanya hii pesa moja kwa moja iende *TARURA* ikatumike kujenga barabara za vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

Wapo wageni wa Mheshimiwa Sylvia Sigula na mmoja ni Afisa Mawasiliano na Miradi kutoka *Global Peace Foundation* Tanzania, na huyu anaitwa Sylvia Mkomwa na mwingine ni Mary Mangu. Karibuni sana. (*Makof!*)

Tunao pia wageni wa Mheshimiwa Emanuel Mwakasaka ambao wanatoka Kanisa la Moravian Tabora,

na hawa ni watoto yatima wameongozwa na Lucas Masanja. Karibuni sana Bungeni watoto wetu. (*Makofii*)

Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa na Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao ajiandae.

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika ahsante. Nijielekeze moja kwa moja, kwenye mchango wangu nianze na Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Sura namba 178. Katika eneo hili kwanza naipongeza Serikali, pia nampongeza Waziri, Mawaziri wote wawili wa Fedha na wa Elimu. Hata hivyo, katika eneo moja tu ingefaa tuishauri Serikali wakati tunakwenda kuipitisha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kunukuu hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kwenye ukurasa wa sita anasema hivi, Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Sura ya 178 inasema hivi; Sehemu ya Saba kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho kwenye kifungu cha 7 cha Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Sura ya 178, ili kuweka mashari kwa Bodi ya Mikopo kutoweka ada au tozo yoyote ikiwemo *value retention fee* kwenye mikopo ya wanafunzi kabla ya kupata idhini ya Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Elimu baada ya mashauriano na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakubaliana nami kwamba, dhamira ya Serikali ni njema sana, lakini hapa kwa lugha ya kisheria, Kiingereza lakini pia ya kisheria, hii inaitwa *clawback clause*. Tafsiri yake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, unapoweka takwa la masharti maana yake unampa mtu haki kwenye mkono mmoja, halafu unamnyang'anya kwa mkono mwengine. Unavyoweka masharti Bodi ipate kibali cha Mawaziri hawa wawili baada ya mashauriano hii ni *clawback clause*, maana yake unatoa haki kwa mkono wa kushoto na unainyang'anya kwa mkono wa kulia.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe tu Mheshimiwa Waziri katika hili, nadhani tupate maelezo hapa. Mapendekezo yangu ni kwamba, tunapotoa katazo la namna hii kwa mujibu wa sheria libaki hivyo ili tusitoe haki kwa mkono wa kushoto na kuinyang'anya kwa mkono wa kulia.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende eneo lingine la Sheria ya Rufaa za Kodi, Sura ya 408, naomba ninukuu tena, ukurasa wa 13 kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Sehemu ya Ishirini na Tatu inapendekeza marekebisho kwenye kifungu cha 22 katika Sheria ya Rufaa za Kodi, Sura ya 404 ili kuanzisha utaratibu wa kufanya usuluhushi wa migogoro ya kikodi nje ya Mahakama. Hoja yangu hapa utaratibu huu ni upi? Huu utaratibu mwagine ambao sasa tunasema tuutumie kuondokana na jambo la kupeleka kesi Mahakamani, nashauri pia, eneo hilli ingefaa tupewe maelezo mengine ya kueleza utaratibu huu husika unakwenda kutumika sasa. Ukitisema tunaandaa utaratibu tu, katika hili tunaacha ombwe. Yamkini sasa tunafuta Mahakama na sasa hatuna rufaa kabisa za kikodi, kwa hiyo atueleze tu utaratibu ambao Serikali inatuletea ni upi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba njielekeze pia kwenye eneo lingine la Sheria ya Kodi za Majengo, Sura ya 289. Naipongeza Serikali, kwanza kwa kupunguza kodi mpaka kufikia Sh.1,000 kwa nyumba za kawaida na kwa nyumba zenye ghorofa kwa maana ya kila ghorofa litatozwa Sh.5,000. Hilo ni jambo jema sana. Hoja yangu ya msingi, ni kweli tunapambana na mapato, changamoto ninayoiona tunapambana na mapato katika vyanzo vilivyopo, yaani hatufungi wigo mpana, hatufikiri tofauti kupata vyanzo vingine vipyta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maelezo hapa ya kuongeza wigo wa kodi, lakini ukiangalia katika uhalisia huoni kodi zipi zimeongezeka, wigo huu ni wa wapi? Vyanzo vipo, naomba nipayo kwenye eneo lingine la Sheria ya Kodi za Majengo, Sura ya 289, naomba nipayo kwenye eneo lingine la Sheria ya Rufaa za Kodi, Sura ya 408, naomba ninukuu tena, ukurasa wa 13 kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Sehemu ya Isha-

mwaka Serikali inapata nini, kwa sababu nayo hay ani mapato yake. Hiki ni chanzo kingine tunakiacha na watu wanakwenda huko wengi, kwenye *apartment* na nyumba za kupangisha wanalipa kodi gani zaidi ya *proper tax*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani pia tuliangalie eneo hili, huku kuna fedha pia, tusiache fedha hizi zipotee, tuishauri Serikali, Mheshimiwa Waziri wa Fedha tuangalie eneo hili hata kama sio leo, basi wakati ujao waone chanzo hiki muhimu, kwenye *tax base*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine nishauri pia ni suala zima la Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 232. Tumeona hapa, naomba niishauri Serikali, kuna kitu tumekiacha hapa. Kuna tozo hii ambayo nadhani pia wananchi wanaumia sana, tozo ya ongezeko la mtaji yaani *capital gain tax*. Unapofanya *transfer* ya jengo au kiwanja unapaswa ulipe asilimia 10 ya kipato ulichokipata. Kwa mfano, mwananchi akiuza nyumba yake kwa bilioni moja anapaswa ailetee Serikali milioni 100, je, nani yupo tayari na mwaminifu wa kiwango hicho? Milioni 100 kuipeleka Serikalini tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naangalia Kenya, wenzetu wanatoza *five percent*. Kwa hiyo, niishauri Serikali kama sio leo kwenye Muswada huu na hii *spoon food for thought*, awamu ijayo watakayokuja, katika eneo hili pia wawapunguzie mzigo Watanzania. Niseme tu kuna *multiplier effect* hapa, ukipunguza *10 percent* ya *capital gain tax* kwenda kwenye *five percent*, utahamasisha biashara ya kwenye sekta ya ardhi, majengo na maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii haitoshi, kwa sababu kwa mfano mwananchi ana kiwanja hawezি kukiendeleza, kuna mfanyabiashara anataka kujenga hoteli anakuja kununua na bahati nzuri sasa *multiply effect* itapatikanaje, atajenga jengo la hoteli tutapata na kodi zingine huko. Kwa hiyo, hata Sekta ya Ardhi kwenye uwekezaji itakua kwa kiwango cha juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, tunao wageni wengine. Wageni watatu wa Mheshimiwa Priscus Tarimo ambao ni watoto wake kutoka Mkoani Kilimanjaro wakiongozwa na ndugu Angelita Priscus. Karibuni sana. (*Makofi*)

Lakini pia wapo wageni 41 wa Mheshimiwa Anthony Mavunde ambao ni watendaji wa kata zilizoko katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma wakiongozwa na ndugu Sostenes Mwera. Karibuni sana watendaji wa kata. (*Makofi*)

Tunao pia wageni 41 wa Mheshimiwa Cosato David Chumi ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotoka Mafinga Mkoani Iringa wakiongozwa na ndugu Ben Lyuvale. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Mharami Mkenge ambao ni Katibu wa Kamati ya Amani ya Wilaya ya Bagamoyo ndugu Ibrahim Gama na Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mpira Mkoa wa Pwani ndugu Cole Mitoso. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao wageni 40 wa Mheshimiwa Jerry Silaa ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu Dodoma wanaotokea Ukonga Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na ndugu Abdulatif Mtoni. Karibuni sana. (*Makofi*)

Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa atafuatiwa na Mheshimiwa Tabasamu Hamisi Mwagao. Mheshimiwa Florent Kyombo ajiandae.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Muswada ulioletwa mezani wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2021 ambao unakwenda sasa kuleta marekebisho na mapendekezo mbalimbali yatakayotuwezesha kutekeleza bajeti tulioipitisha hapa juzi na ambayo Watanzania kwa asilimia kubwa wameiunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utakuwa mdogo sana kwa sababu ningependa tu kuchangia juu ya Sheria ya Kodi ya Mapato Namba. 332 na Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta Sura ya 220. Lakini kabla sijachangia hoja zangu mbili katika haya maeneo nilipenda tu nitoe ushauri wa jumla na mtazamo wangu kuhusu dhana ya kulipa kodi katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli mimi nilivokuwa nikiwa mdogo na nikitafakari jinsi kodi inavyochukuliwa katika Taifa letu na labda Mataifa yanayoendelea ni kwamba watu hawapendi kulipa kodi na inawezekana watu hawailewi umuhimu wa kulipa kodi na kwa sababu pia nimebahatika kupata *exposure* ya kuishi nchi za wenzetu kila raia anajua umuhimu wa kulipa kodi na kulip akodi ni wajibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini inawezekana pia historia tuliyonayo ni kwamba watu walikuwa hawaoni faida ya kulipa kodi na ndiyo maana wengine wanathubutu kukwepa wanasema hata nikilip ambona bado sina barabara, sina maji, sina umeme. Lakini dhana hii nadhani katika hizi awamu mbili zilizofuatana, Awamu ya Tano ya Serikali yetu na Awamu hii ya Sita kila Mtanzania ni shahidi kwamba mapinduzi makubwa ya ukuaji wa uchumi wet una miundombinu yake ni ushahidi wa kutosha kwamba kodi zetu zinapolipwa zinafanya kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nipende kuwashauri Watanzania kwamba tusione kodi kama ni mzigo na kama ni msalaba ambao tunapikwa bila sababu ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo ninapenda pia kuishauri Serikali ijikite katika kuanzisha kampeni kubwa ya Kitaifa ya kutoa elimu ya kodi na isiishie tu katika kutoa elimu ya kodi ikiwezekana iwekwe pia katika mitaala ya elimu kuanzia elimu ya msingi kwenda juu lakini zaidi ya hayo Serikali iweke mkakati wa kusambaza kodi ili kila mtu mwenye hadhi ya kulipa kodi aweze kugawiwa sehemu yake kulingana na kipato chake alipe kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukifanya hivyo, tunaweza tukapunguza mzigo wa kutwisha kodi kubwa kwa baadhi ya watu wachache ambao ndiyo wanalipa kodi katika nchi yetu watu ambao hawafiki hata 5,000,000 ili mzigo upungue na kila mtu alipe kodi kwa kufurahia kama ambavyo waumini katika madhehebu yao huwa wanatoa sadaka kila Jumapili au Ijumaa kwa kufurahia tena bila kulazimisha na mtu ye yote. Kuna Fungu la Kumi, sadaka ya kwanza na ya pili na sijawahi kuona muumini akilalamika. Wanatoa kwa sababu wanaamini kuna baraka wanayokwenda kupata kwa Mwenyezi Mungu. Sisi tunakwenda kupata baraka kwa kukuza uchumi wetu, miundombinu yetu, elimu yetu na afya yetu tunapotoa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo basi sasa nichangie zile hoja zangu mbili katika hiki Kifungu cha 25 ya Muswada wa Sheria ya Fedha 2021 ambapo kuna kodi ya zuio la asilimia 2 katika mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi. Nimesoma pia maelezo ya Waziri akisema kwamba kodi hii haitawagusa wafanyabiashara wadogo, vyama vya ushirika, inakwenda kwa mawakala na makampuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaomba nijiridhishe na baadae atakapokuja kuhitimisha anisaidie kufafanua kwamba ni kwa jinsi gani atawalinda hawa wadogo wasio na kipato. Kwa mfano, kuna viwanda hivi sasahivi vinajengwa sehemu mbalimbali nchini za kuchakata mazao ya mifugo. Sisi tuna kiwanda katika Wilaya ya Longido cha kuchakata nyama za mifugo. Adha ambayo tumepata tangu kiwanda hiki kianze ni adha ya bei anayonunulia yule mwenye kiwanda mifugo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikafika mahali tunamuomba afanye utafiti na nchi ya jirani watu walikuwa wanapeleka mifugo mingi Kenya tunakosa mazao mengine yanayotokana na nyam ana ikafika mahali na yeye akaona akaanza kupandisha pole pole bei ya kilo ya nyama lakini malalamiko yake makubwa ni kwamba kodi ya Serikali ndiyo kikwazo. Kulikuwa na uititiri wa kodi nyingi ambazo hata sijaona kama

zimeshapunguzwa kwa jinsi ambavyo tumekuwa tukilia katika Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mwekezaji nae kutambua umuhimu wa kuongeza ongeza bei ili asikose malighafi ikafika mahali kilo ya nyama ya mbuzi imefika mpaka 7,500 kutoka 6,500 lakini kwa wenzetu nchi ya jirani ni 8,500. Sasa akiona kwamba kuna hii kodi ya zuio la asilimia 2 isije ikatokea kwamba sasa na yeze ama ata-freeze bei hatapandisha tena bei ya bidhaa ya mfugaji ambayo ni mifugo yake ama ataihamishia sasa kwa mfugaji mwenyewe kuhakikisha kwamba sio yeze anayelipa, anakwenda kupunguza bei ya kununulia ile mifugo ili yeze asipate hasara ya hiyo kodi ya zuio.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningeomba Serikali iangalle namna ambavyo itamhakikishia huyu mfanyabiashara mdogo wa mifugo au mkulima au mvuvi kwamba hizo kodi za zuio asilimia 2 haitakwenda kuhamia kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu wa pili kwenye hii Sheria ya Ushirika, ushuru wa barabara na mafuta sura 220 ni ushauri natoa hapa kwamba kwa sababu tuna TARURA na kwa sababu mfumo wa ukusanyaji wa mapato yetu fedha zote zinakwenda kwenye Hazina kuu ya Serikali ningeomba na nimesoma pia kwenye Taarifa ya Kamati ya bajeti kwamba wangeomba kuwe na mfuko maalum mahsus kwa ajili ya kupokelea hizi fedha zinazokwenda kupatikana kwenye mafuta ya aina zote ambazo zinakatwa shilingi 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, huo mfuko ni muhimu sana na tusiishie tu kuwa na mfuko muhimu kwa sababu itakata ile urasimu wa kwenda kuomba fedha mpaka zitoke HAZINA inachukua muda. Kuwekwe pia na Fungu la dharura litakalopelekwa katika kila Halmashauri ili inapotokea dharura mvua imenyesha daraja limekatika barabara fulani haipitiki, badala ya kuingia mlolongo mzima wa kuomba fedha kule Hazina au labda sasa kwenye huu mfuko wawe na fungu

Iao la dharura kila wakati. Wawe na fungu ambalo watalichomoa tu watengenezee miundombinu iliyoharibika kama mfuko wa dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria itambue hilo na marekebisho mwende mparekebishe kidogo kuwe na *percent* kulingana na mahitaji ya barabara zilizoko katika kila halmashauri ili halmashauri ziweze kuwa na mfuko wake wa dharura wa kunusuru barabara zinapoharibiwa na mvua kwa sababu barabara nyingi ambazo hii fedha inaenda kusimamia kwa asilimia kubwa zitakuwa bado ni zile barabara za changarawe, barabara za udongo ambazoni rahisi sana kuharibiwa na mabadiliko ya tabianchi inaponyesha mvua wakati wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache napenda kuwapongeza tena Wizara hili ya Fedha na Mipango kwa bajeti nzuri waliyotuletea na hata kwa huu muswada na marekebisho yanayopendekezwa lakini wana kazi kubwa ya kutoa elimu ya kodi na sio elimu ya kodi tu na kufanya marekebisho mbalimbali ambayo Wabunge wenzangu wametangulia kuyasema ili utekelezaji wa hii bajeti ya mwaka 2021/22 uweze kuleta tija ambayo Watanzania wanaitegomea. Ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nashukuru. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Tabasam Hamisi Mwagao atafuatiwa na Mheshimiwa Florent Kyombo, Mheshimiwa Zahoro Mohammed ajiandae.

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi kuchangia Muswada wa Sheria ya Mabadiliko katika Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hiki Kifungu cha 16 (47) ambacho kinazungumzia suala la *TARURA* la hizi fedha shilingi 100 ambazo zinakusanya. Sasa pesa hizi ni kwamba zilipigwa kelele na Wabunge na wakaomba mahali gani pa kutoa pesa hizi na tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kukubaliana na Wabunge wenzake na kuona kuna

umuhimu wa kutengeneza hizi barabara. Najua na yeye katika Kifungu hiki atatengeneza barabara zake katika maeneo mengi katika Jimbo la Iramba. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika jambo hili kuna hii asilimia 30 kama inavyozungumzwa na Wabunge wengine ilikuwa ni shilingi 78.90 kwa hiyo ikichukuliwa hii shilingi 78.90 na ikajumlishwa shilingi 100 ikawekewa *ring fence* kwa siku kwa uuzaaji wa mafuta lita milioni 12 kwa siku tuna uwezo wa kupata bilioni 2 na milioni 148 kwa siku pesa ambazo zitakwenda *TARURA* na kwa mwezi tunapata zaidi ya milioni kama bilioni 64 hivi. Kwa mwaka inaonesha tuna uwezo wa kupata bilioni 778. Sasa bilioni 778 haziwezi kuachwa hivi hivi, hiki ni kitu kikuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba, ushauri wetu sisi ni kwamba huku kwenye pesa hii ambayo itabakia ya *TANROADS* wana shilingi 184.10 na *TARURA* tutakuwa na shilingi 178.90 inamaanisha kwamba Bodi iliyoko pale ya Mfuko wa Barabara bodi hii inaundwa na Waziri wa Ujenzi isipokuwa mtu mmoja tu anayeteuliwa na Mheshimiwa Rais. Sasa wana mfuko wao wao na wana bodi yao, sisi ambao tumepiga kelele kwa sababu ndiyo tunakokaa na wananchi kule vijijini na sisi tunaomba katika sheria hii iundwe Bodi yet una Mfuko wetu ili kumfanya Waziri wa Serikali za Mitaa aweze kuwajibika na hizi pesa kwa sababu wale wajumbe wa Bodi yeye ndiyo mteuzi wake lakini atateua jina ambalo litakwenda kupitishwa na Mheshimiwa Rais ili sisi tuwe na uhuru na hizi pesa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasahivi Serikali za Mitaa ni kwamba hawana Bodi yao hawa watu wa Serikali za Mitaa kwa ajili ya barabara za vijijini na hawana mfuko wao. Itawekwa *ringfence* tu peke yake lakini Mfuko haupo. Kujua usalama wa hizi pesa bado kutakuwa na mgogoro baadaye. Sasa hii shilingi 30 tuhakikishiwe na Waziri wa Fedha akija hapa kwenye majumuisho tujue sasa kama hii shilingi 30, shilingi 78 na shilingi 100 zote zinakwenda *TARURA* na ziweko kwenye sheria hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jingine hili suala la sheria hii ambayo inakuja kuingia, hii Sheria ya *withholding Tax*, sheria hii inaleta kidogo kigugumizi kwamba mwananchi anakwenda kuza mazao yake iwe samaki au ni embe au chochote kuza kiwandani akatwe hizi pesa na wakati huo amelipa ushuru kutoka kwenye halmashauri husika.

Kwa hiyo, huyo mwananchi ambaye ni mkulima au mvuvi atalipa kodi mara mbili. Hii asilimia 2 sio ndogo, ni nyngi na kama anauza kila mwezi kwa mwaka anakwenda kufanya jambo hili haya malipo yatakuwa makubwa sana kwake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfanyakia shara mkubwa, hii *withholding tax* kwake sio shida kwa sababu atauza na siku akienda kufanya hesabu zake za kulipa kodi Yam waka atakata hizi *withholding tax* atapeleka pale kuonesha katika hesabu. Haya huyu mkulima atapeleka wapi? Kwa hiyo, analipa ushuru katika Halmashauri husika na anakwenda kulipa tena *withholding tax* huko Serikali. Tunaomba tu kwamba tuisiwakatishe tamaa hawa wakulima wetu. Wanaanza kuona kodi zinakuja hizi inakuwa ni mtihani kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, tuisitie mchanga kwenye kitumbua ambacho umekipika vizuri sana. Yaani leo wananchi wanashukuru sana bajeti hii. Wakisikia tena kuna kodi wanawekewa hii italeta shida naomba tu uje uielezee vizuri ili wananchi huko vijijini waone kwamba kazi tunayokwenda kuifanya katika Serikali hii basi na yenye kazio inaenda kuwapa manufaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo nashukuru sana, nakuunga mkono sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kwa hii bajeti yako na kama huu ushauri wetu utausikia kuunda Bodi yetu ya TARURA kule na Mfuko wake uende kule hongera sana Mungu akujaalie sana katika hii miaka mitano ya utendaji wako kazi. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Florent Kyombo atafuatiwa na Mheshimiwa Zahoro Mohammed, Mheshimiwa Eric James Shigongo ajiandae.

MHE. FLORENT L. KYOMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa nafasi. Kwa nafasi ya pekee nishukuru Serikali yetu kupitia Wizara yetu ya Fedha kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba pamoja na wasaidizi wake kwanza kwa kuleta mpaendekezo ya maeneo gani ambayo Serikali inaweza kukusanya fedha na tukaweza kuzipata kwa ajili ya shughuli mbalimbali za maendeleo katika nchi yetu. Hiyo tunaiona kwa kuthibitisha kupitia huu Muswada wa Fedha ambaao utasaidia utekelezaji sasa wa hayo maeneo ambayo ni mapya katika ukusanyaji wa fedha hizo uweze kufanyika kwa urahisi lakini pia kufanyika kwa mujibu wa sheria za nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo machache tu katika maeneo machache pia ni ushauri ili kuendelea kuboresha ili utekelezaji wa maeneo haya uweze kusaidia kwenda vizuri lakini pia na kuweza kupunguza matumizi mengine ambayo yanaweza yakawa ni makubwa zaidi kuliko ambavyo tungeweza kushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la Sheria ya *Local Government* kwenye eneo ambalo sehemu ya 9 ambayo imeonesha marekebisho mbalimbali lakini pia kuna suala la ushuru wa sehemu za maegesho kupitia *TARURA* ambayo imekuwa ni chanzo kizuri cha fedha kwa ajili ya kuongeza fedha hizo kwa ajili ya kuchangia ujenzi wa barabara zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hilo naunga mkoo hoja mapendekezo yote ambayo Serikali imekuja nayo lakini kuna maboresho jinsi ya utekelezaji wa sehemu hiyo ambayo kimsingi naamini Serikali hii ni moja inafanya kazi moja. Nikiangalia kwa undani *TARURA* ni taasisi ambayo imeanzishwa muda si mrefu kwa hiyo hata *manpower (Resource)* ya watu iliyonayo na baadhi ya section katika Taasisi hiyo bado inakuwa ni changa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuna maeneo mengine ambayo nakuwa naona kwa kuwa Serikali ilishaweka miundombinu hasa katika *Local Government* kuanzia katika ngazi ya wilaya mpaka ngazi ya kitongoji ambazo zote mfumo uko vizuri katika usimamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchango wangu katika eneo hili nilikuwa nashauri fedha hii ya maegesho ni kweli iendelee kuwa ni fedha ambayo inakusanya kwa ajili ya *TARURA* lakin *means* ya kukusanya zile fedha ningeshauri Halmashauri ingekusanya hizo fedha kwa niaba ya *TARURA* na hizi fedha sasa zikaelekezwa kwa mfumo mzuri wa kisheria zikawa zinapelekwa kwa ajili ya kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme ni kwa sababu gani? Kwa sababu, kitu cha kwanza halmashauri inazo posi ambapo posi hizo zinatumika kukusanya mapato yote na katika posи hiyo unaweza ukaweka *provision* nydingi za ukusanyaji wa mapato hata kama yakiwa ni mapato zaidi ya 1,000. Lakini halmashauri hizo hizo zinazo *manpower* mpaka ngazi za mitaa, ngazi za vitongoji na vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia katika wilaya zetu *structure* ya wilaya, tuachane na zile wilaya ambazo ziko katika miji mikubwa labda manispaa. Halmashauri zingine za wilaya zina visehemu vidogo vidogo vinavyokua kimji kwa hiyo unakuta *TARURA* yenyewe huwa inawezekana kukusanya maegesho katika eneo la Mji Mkuu lakini huku ambako ni mji mdogo ambao umechangamka na *parking* zipo za magari unakuta maeneo hayo ukusanyaji unakuwa ni mgumu kwa sababu gani, kwa sababu *TARURA* haina watu wa kutosha kusimamia katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia, hata *TARURA* ikijielekeza *ku-out source* kwamba imeingia na kampuni gharama ya usimamizi au kuilipa ile kampuni kukusanya zile hela ndogo zinazopatikana katika maeneo ambayo ni pembezoni mwa miji ni kubwa kuliko hata makusanyo yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa pili ni kuipongeza Serikali hasa kwa upande wa ukusanyaji wa *Property Tax* ambapo katika mchango wangu wa awali nilisema ilikuwa ni eneo lilioshindikana. Nimshukuru Mheshimiwa Waziri kuja na mawazo mazuri na njia iliyotumika ni nzuri na sahihi. Nimeshukuru kuona katika kifungu hiki imeongezwa kwamba asilimia 15 ya fedha hizi zitarudishwa katika Wizara husika ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa kama gawio la Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili ni zuri kwa sababu tunajua haya maeneo yako ndani ya halmashauri zetu lakini halmashauri lazima iendelee kutenga na kuboresha makazi ya wananchi wetu. Kwa hiyo, kurudisha hii fedha itasaidia sasa Halmashauri kuendelea kufanya kazi ambayo ilikusudiwa. Pamoja na kukusanya *Property Tax* lakini basi tuendelee kuboresha maeneo hayo illi sasa wananchi wetu waone kile wanachokichangia, fedha inapoenda Serikalini inarudi na kuendelea kuboresha maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo langu la mwisho nataka kushauri, kwenye *Bill* hapa sijaiona vizuri, lakini niombe kama ambavyo wamefanya katika *Property Tax* kwenye asilimia 15 na hili suala la wajasiriamali ambao wanatumia vitambulisho tuliangalie. Wajasiriamali wetu wanafanya kazi katika magulio na katika masoko na katika hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri tunaenda kuwapa vitambulisho ambavyo vinawasaidia kwa kweli, wanalipa Sh.20,000/= wanakuwa hawasumbuliwi, lakini ni jinsi gani halmashauri inaenda kuboresha yale maeneo ambayo wajasiriamali wetu wanafanya biashara zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba kama ambavyo tumefanya kwenye *Property Tax* tunaweza tukaona namna gani gawio kidogo linalotokana na makusanyo ya vitambulisho vya wajasiriamali likarudi tena kule halmashauri ili basi waendelee kuimarisha magulio na masoko ili sasa wananchi wetu wafanye kazi au biashara zao katika mazingira ambayo ni rafiki. Iwekwe miundombinu ya vyoo na maji na huduma nyingine za kijamii zinazotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili nilitaka kuchangia hayo machache. Nakushukuru kwa nafasi na naunga mkono Muswada wetu uweze kupita kwa kishindo. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Zahoro Mohammed, atafuatiwa na Mheshimiwa Eric James Shigongo, Mheshimiwa Juma Usonge Hamad ajiandae.

MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru. Mimi napenda kuchangia kitu kimoja tu, lengo la Serikali yetu hii ni kuhakikisha kwamba tunaondoka tulipokuwepo tunapiga hatua za mwendokasi ili kuhakikisha wananchi wanayaona na wana-*feel* maendeleo ambayo Serikali yao imeamua kuyafanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimewasikia Waheshimiwa Wabunge wengi hapa wakizungumza juu ya maendeleo au mikwamo ya maendeleo inayotokana na jitihada za wananchi, hasa wakulima wetu. Mapendekezo yalitoka hapa na moja ya eneo ambalo bado hatukui, kila siku tunaendelea kupiga *mark time*, ni eneo hili tunaloliita la *road and fuel toll*, maana yake ni nini? Ukiangalia *statistics* za matumizi yetu ya mafuta kwa miaka yote hatukui, leo tuna miaka saba, lakini magari yanaendelea, kampuni zinakuja, mafuta yanatumika, lakini hesabu zinaonekana tuko palepale hatukui. Maana yangu ni nini, tunalo tatizo kwenye hesabu zetu au kwenye *statistics* zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Serikali imeleta maboresho, kwanza mnisamehe mimi si mwanasheria *by profession*, naomba nisome hiki ili nitafsiri kwa lugha isiyo sahihi au isiyo *official*. Kifungu 47 kinasema:

"The principal Act is amended in section 4A by deleting paragraph (a) and substituting for it the following:

"(a) Tanzania shillings 363 per litre imposed on petrol or diesel shall be deposited into the account of the Fund:

Provided that, Tanzania shillings 100 per litre imposed on petrol or diesel out of the Tanzania shillings 363 per litre shall be allocated to Tanzania Rural Roads Agency and the remaining Tanzania shillings 263 per litre shall be distributed amongst the Fund and the Tanzania Rural Roads Agency in the manner prescribed in the regulations made by the Minister in consultation with the Minister responsible for local government."

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni nini? Tumekusudia kuondoka tulipokuwa kwenye shilingi 263. Waheshimiwa Wabunge wameomba tuongeze shilingi 100 iwe shilingi 363. Kwanza shilingi 100 hii imewekwa makusudi iende TARURA peke yake, lakini katika shilingi 263 tunayo shilingi 78.90 ambayo na yenye we inarudishwa kwenye hii ili tuwe na shilingi 178.90 ili tuweze kupiga hatua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwenye hili ningemba sana kusiwe na mchanganyiko hapa kwamba Waziri kwa kushauriana na nini, hapana. Tuiseme categorically kwamba shilingi 178.90 inakwenda kutumiwa na TARURA full stop. Tusiwape watu nafasi ili tuweze kuja kujitathmini kwamba tulipata hela hii tukaiweka hapa ili ifanyiwe kazi na TARURA. Tusimpe mtu mwengine nafasi ya kuweza kuamua kuwapa au kutokuwapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mchango wangu mimi kwenye hili ni kuipongeza Serikali kwa kusikiliza Wabunge, lakini kuliomba Bunge lako hili tuzungushe wigo hapa tusimpe mtu nafasi ya kuamua yeye. Sisi tumeamua utekelezaji ukafanywe moja kwa moja. Nakushukuru. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Eric James Shigongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Usonge Hamad, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Mcemba Madelu ajiandae.

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu mchana huu wa leo. Hoja yangu kubwa itakuwa

kwenye suala zima la *Transfer Pricing*. Jana suala hili limenifanya sikulala vizuri usiku. Nimelala natafakari, nafikiria namna ambavyo nchi yangu inaibiwa fedha nyingi na wajanja wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilifanya utafiti kidogo, kwanza nilitaka nijelimishe hivi hawa watu wanatuibiaje? Nikaja kugundua kwamba hawa watu wanatuibia kwa namna mbili, kama ambavyo ametangulia kuzungumza Mheshimiwa Yahya ni kwamba kampuni inakuwepo hapa Tanzania labda ni Geita kunakuwa na kampuni nyingine Dubai na kampuni nyingine Mauritius. Kwa mfano kama ni dhahabu inayochimbwa na Shigongo ambayo ni kampuni iko Tanzania anamuuzia aliyeko Dubai, ili kuikosesa Tanzania mapato anaiza kwa bei ya chini, badala ya Sh.100/= anaiza kwa Sh.10/= ili awaoneshe kwamba aliuza kwa hasara. Anapotaka kununua *spare parts* zake ananunua kwa kampuni yake nyingine iko Mauritius inamuuzia *spare parts* kwa bei ya juu ili kusudi aonekane gharama zake za uendeshaji zilikuwa kubwa aoneshe hasara ili Serikali isiweze kupata kodi. Huu ni wizi na wizi wa namna hii hauwezi kuvumiliwa, nchi yetu haiwezi kuendelea kupoteza mapato. Wenzetu wazungu wanaandaa utaratibu huu kwa nia moja tu ya kuzibbia nchi za Afrika ziendelee kuwa masikini nao waendelee kujitajirisha. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Taifa hatuwezi kuruhusu mambo haya yaendelee na nataka nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa sheria ambayo ameileta hapa Bungeni. Ameleta hapa kipengele ambacho kinataka kufanya *adjustment* kidogo kwenye sheria yetu. Kinasema kwamba tukishamkamata huyu mtu katuibia asilimia 30 yetu kama kodi atulipe, akishatulipa asilimia 30 tumpige asilimia 100 kwenye zote alizokuwa ametuobia. Sasa hatuwezi kuondoa 100 ambayo ni *fine* kwa lengo tu la kuwaita eti waje kuwekeza nyumbani kwetu, hawa sio wawekezaji hawa ni wezi; hawa ni wezi hatuwataki. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kimoja ambacho najua kimempa changamoto Mheshimiwa Waziri ni kwamba wakati

anatakiwa kuwabana wawekezaji wakati huohuo anatakiwa aboreshe mazingira wawekezaji waje, kwa hiyo, amejikuta yupo njia panda. Akaja na *solution* ya kwamba kwa sababu niko njia panda nifanyeje wawekezaji waje ili niweze kupata kodi, uchumi wetu unakua kwa asilimia 4.5 kwa sasa, akajikuta anasema nipunguze angalau tutoke asilimia 100 ya *penalty* iwe asilimia 75. Mimi nakubaliana na asilimia 75 ambayo Mheshimiwa Waziri ameona inafaa na naomba kabisa kama lengo ni ku-*attract investors* tuwapige asilimia 75 na wakati uleule tuwapige asilimia 30 ya kodi walivyokuwa wanatuibia. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba Kitengo chetu cha *International Tax Unit* cha *TRA* hakina uwezo wa kuwakagua wafanyabiashara wote. Hakina uwezo wa kuzikagua hizi *multinational* zote zilizoko hapa nchini, hakina uwezo, kina wafanyakazi 18 tu mpaka ninavyozungumza hivi sasa. Wafanyakazi 18 hawana uwezo wa kukagua kampuni zote hizi.

Ombi langu mimi kwa Mheshimiwa Waziri ni kwamba *waki-strengthen* Kitengo hiki kiwe na nguvu, wafanye *capacity building* ya kutosha watu hawa wawe na uwezo wa kukagua kampuni zote zilizoko hapa nchini ambazo ni *multinational* ili tuweze kugundua matatizo yote ambayo yanafanyika na wizi wote ambao unatokea. Tukishawakamata hatuna huruma, ni kodi yetu asilimia 30 na asilimia 75 yetu tuwatoze. Watakaotaka kufanya biashara wafanye ambao hawataki kufanya biashara na sisi waondoke. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nikukumbushe jambo moja la muhimu sana ya kwamba viwanda vyetu vya alizeti vya kukamua mafuta vikumbukwe. Viwanda vikubwa vinapata *zero eighteen percent* ya VAT, viwanda vidogovidogo vinapigwa asilimia 18. Naomba Mheshimiwa Waziri awakumbuke wafanyabiashara wadogowadogo wenye viwanda hivi nao pia waweze kupatiwa *zero eighteen percent* nao waweze kufaidi soko letu la alizeti hapa Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kushukuru sana na baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Juma Usonge Hamad, atafuatiwa na Mtoa Hoja, Waziri wa Fedha na Mipango.

MHE. JUMA USONGE HAMAD: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia kwenye Muswada huu wa Sheria wa *Finance*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyofahamu sasa hivi tuko kwenye harakati za kurudi majimboni. Mimi kama Mbunge ambaye natokea Zanzibar kwenye Jimbo la Chaani naamini kwamba kutakuwa kuna maswali kwa wapiga kura wangu, lakini sio tu kwa wapiga kura wangu hata wafanyabiashara au watu ambao wataguswa na Muswada huu wanaweza wakauliza. Zanzibar ni ndogo, kwa hiyo, naamini kufikika kwangu ni rahisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nijielekeze moja kwa moja kwenye Muswada huu kwenye *Amendmentya Value Added Taxes, Cap. 148, amendment ya Section 3*, kuna kipengele namba 2, 3 na 4 ambapo tunazungumzia suala la ongezeko la VAT kwa wafanyabiashara kuchukua bidhaa kutoka Tanzania *Mainland* kwenda Zanzibar na Zanzibar kuja Tanzania *Mainland*. Sasa hivi kuna mapendekezo mapya ya sheria kwa mfanyabiashara kutoka Zanzibar akichukua *product Bara* kupeleka Zanzibar au wa Zanzibar akichukua *product* kuleta Bara atatozwa asilimia 18, naona hatujaenda *in deep* zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Zanzibar ipo sheria ambayo inatambua mfanyabiashara akitoa bidhaa aidha *import* au *consumption* anatozwa asilimia 15 kule Zanzibar. Hata juzi tu Baraza la Wawakilishi limemaliza sijaona Muswada huu wa Sheria na leo hii Muswada wa Sheria umekuja huku, sijajua mantiki ya hii itakuwaje. Maana Zanzibar ukichukua bidhaa kule ukisema utokenayo unatozwa asilimia 15, Bara tunaambiwa asilimia 18, sasa akitokea mtu ambaye

anasafirisha bidhaa anatozwa asilimia 18, sijui sheria ipi kwa kule kwetu Zanzibar itakuwa inamruhusu kwamba *ZRB* au *TRA* atamkata huyo mfanyakishara asilimia 18 kwa sheria ipi? Maana ni kwamba tunawaongeza Mamlaka ya Mapato ya Zanzibar asilimia tatu ya ziada.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atupe ufanuzi juu ya suala hili ili tuondoe mkanganyiko na zisije zikaibuka changamoto za kusema kwamba Muungano huu una shida ingawa Muungano wetu ni mzuri na Mama ameonesha nia njema kabisa ya kuimarisha Muungano huu ambao unatupa fursa sisi kama Watanzania kutembeleana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la pili, Zanzibar kuna Bodi ambayo inashughulika na masuala ya kukagua bidhaa ambayo tunaita *ZBS* na huku Bara kuna mamlaka nyininge ambayo inaitwa *TBS*. Kuna changamoto nydingi ambazo zimeshajitokeza, kuna bidhaa ambayo inazalishwa kule Zanzibar inapewa logo ya *ZBS* (*Zanzibar Bureau of Standards*) na huku Bara ipo. Kwa hiyo, nina wasiwasi inawezekana kuna wafanyakishara ambao wamekuwa *interested* kuja Zanzibar kuchukua bidhaa lakini mwisho wa siku wakaja kukutana na kikwazo hiki cha Shirika la Viwango. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nahitaji pia maelezo kidogo ili mradi tuondoe huu mkanganyiko baina ya nchi zetu mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, kwenye kipengele namba 4 tunaambiwa fedha zitakazopatikana zitaenda moja kwa moja kwenye Hazina ya Zanzibar; zitakazopatikana huku Bara kwa wale wafanyakishara ambao watatozwa hiyo asilimia hiyo 18 zitaenda kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina. Katika sehemu ambayo wafanyakishara wengi wanalamika ni kuhusiana na fedha ambazo zinakwenda Hazina kurejeshwa Zanzibar zinakuwa na changamoto kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Wizara iweke angalau sheria ambayo itaweka wazi na *time limit* ili kama kuna fedha ambazo zinatakiwa zirejeshwe Zanzibar basi kuwe

kuna muda ambao fedha zinatakiwa zirejeshwe, ile *returning* ya fedha nadhani itakuwa ni jambo zuri Zaidi. Hapa tunaambiwa kwamba fedha ambazo zimepatikana Zanzibar zirejeshwe Bara na za Bara zirejeshwe Zanzibar lakini hakuna muda, inaweza kuja kuibua hoja nayo ikaleta shida kabisa. Kama nilivyotangulia kusema kwamba Muungano huu ni mzuri, utaendelea kuwa mzuri. Mama ameonesha nia njema kabisa, nadhani Tanzania tunaenda kupiga hatua nzuri na uchumi wetu utaimarika vizuri zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la nne, kuna suala linazungumziwa sana kuhusiana na sukari ya Zanzibar, lipo hilo, ingawa VAThii nayo pia imeenda kugusia zaidi. Itaenda kufungua mwanya wafanyabiashara kule au kile Kiwanda cha Sukari cha Zanzibar nacho kitawezeka ku-supply huku Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kutokana na tozo hii mpya ya asilimia 18 nina wasiwasi mkubwa sana kwa sababu huyu mfanyabiashara, yule *manufacture* wa sukari wa Zanzibar akifanya *deduction* yote ya kutoa gharama za malighafi alizotoa nje kwa ajili ya *import*, inaweza ikasababisha mfanyabiashara kutoka Bara akiwa *interested* na kuja kuchukua sukari Zanzibar gharama ya sukari ya Zanzibar inawezekana kuwa kubwa zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweza tukaja kufungua mianya ya wafanyabiashara sasa waache kununua kwenye soko la Zanzibar au la ndani ya nchi zetu hizi wakaenda kuhamia soko la nje. Kwa hiyo, naiomba sana Wizara inipe maelezo mazuri, lakini pia mapendekezo nimetoa Wizara iangalie sheria hii ili baadaye isije ikaleta vikwazo zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, nashukuru kwa kunipa fursa. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nimuite sasa Mtoa Hoja, Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Mchemba Madelu aje ahitimishe hoja yake.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nitumie fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuhitimisha hoja hii. Pili, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao makini kabisa waliyoitoa. Tatu, niishukuru sana Kamati ya Bunge ya Bajeti inayoongozwa na Mwenyekiti, ndugu yangu Mheshimiwa Daniel Silo Baran pamoja na Makamu wake Mheshimiwa Kigua, Mbunge wa Kilindi pamoja na wajumbe wote kwa ushirikiano, lakini pamoja na ushauri waliotupatia na uchambuzi ili kuweza kufanikisha kukamilisha jambo hili katika hatua hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli hii ambayo tuunaendelea nayo ni ya kutunga Sheria ya Fedha. Pamoja na kwamba tunatunga sheria lakini jambo la kwanza la msingi ambalo naendelea kulisisitiza ni wananchi wote kutambua umuhimu wa kutimiza wajibu. Sheria tunajiwekea tu kama kuwekeana miiko na mipaka, ili tuweze kuenenda tunawekeana miongozo lakini kubwa la kwanza ambapo ndiyo sheria ilioandikwa kila mtu moyoni mwake ni yeye kujitambua kutimiza wajibu wake kwa Taifa lake. Hili ni jambo la msingi ambalo mara zote tutaendelea kulisema.

Nawaomba Waheshimiwa Wabunge kwa sababu sisi ni viongozi tuendelee kutembea na kauli mbiu hiyo kwamba watu wetu lazima watembee kizalendo, watembee wakijua wanahitaji kutimiza wajibu kwa Taifa leo, mara zote walikumbuke jambo la aina hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii sio nchi ya viongozi na wala haitajengwa na viongozi tu, ni nchi ya Watanzania wote na inatakiwa kujengwa na Watanzania wote. Pamoja na kwamba tuna kitengo cha kutoa elimu pale Mamkala ya Mapato, kinawakumbushia watu, lakini sisi kama Wizara tumeendelea kuongea na wenzetu wa Wizara ya Elimu kuuona umuhimu kwamba tunakijenga vipi kizazi cha nchi yetu tangu wakiwa wadogo waelewe masuala haya ya wajibu, uzalendo na masuala ya kodi na masuala ya kupinga rushwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hapa ndani tunawapongeza Wabunge ambao wameona taswira ya aina hiyo, Kalumbu Suma nilikusikia uki sema tunaonaje jambo la kodi hili lingewekwa kwenye Shule ya Msingi? Nimemsikia na ndugu yangu Mheshimiwa Kiruswa na wengine walileta kwa maandishi, nilipokea ya Mheshimiwa Oliver. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo ni kubwa. Nilipokuwa mdogo; sasa hivi nimekua kidogo, nilipokuwa mdogo zaidi, wakati tunasoma vile vitabu na kuelezezia na tukiwa tunazisikia nyimbo za wapiganaji walitoka Vita vya Kagera, walikuwa wanatuimbia, "mimi Amini akifa, siwezi kulia. Wakatuonesha na vile vitabu vya kwanza, tunajifunza kusoma, vinaonesha Amini amebeba vichwa vya watu hivi. Katika umri ule nilijua kabisa kwamba yule bwana alikuwa anabeba vichwa, kama tunavyobeba maji vijijini, kwamba unabeba begani, kibuyu kingine kipo mbele, kingine nyuma. Kwa hiyo, nilli meza kama ilivyo kwamba huyu alikuwa anabeba vichwa vya watu hivyo. Kwa hiyo, nikaichukia hivyo na nilikuwa nimehamasika hivyo, kwamba huyu akifa siwezi kulia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, ninachomaanisha ni nini? Watoto wetu tukiwaambia tangu wadogo wakaanza kuona ni aibu kukamatwa kwenye masuala ya kukwepa kodi, tangu wapo shulenii kama alivyosema Mheshimiwa Suma na ndugu yangu Mheshimiwa Kiruswa hapa, tangu wapo shulenii wakaanza kuona kwamba ukionekana unakwepa kodi ni jambo la aibu, yaani ni jambo la aibu kwenye familia yenu; ama mambo ya rushwa ni jambo la aibu kwenye familia yenu, wakajua wangali wadogo, Taifa litakalojengwa na kikazi cha aina hiyo, litakuwa bora sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ilivyo sasa hatujafikia sana hatua hiyo watu kuona kukwepa kodi kama ni jambo baya, wala hatujafikia hatua hiyo watu kushiriki kwenye mambo ya rushwa kuona kama ni jambo la aibu. Hata wengine wangali wadogo wanadhania ni jambo jema. Kuna rafiki yangu mmoja ningali ofisini alikuwa anasema Taifa letu lina safari

ndefu sana kwenye mambo ya rushwa. Mwanae alifanya mtihani kwenye shule moja binafsi ya kutafuta nafasi ya kujinga na chekechea, madarasa ya awali haya ya chini, akakosa. Akawa anamwambia mama yake, yaani tumekosa hii nafasi mama, yaani hata ukiwapa fedha hawataniruhusu! Yaani bado yupo ngazi ile, anamwambia mzazi wake, hivi hata ukiwapa fedha hawataniruhusu! Maana yake hivi vitu vinaanza kujengwa tangu mwanzo kwamba unaweza ukavifanya tu hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili jambo kulifundisha kuanzia watoto wangali wadogo ni jambo ambalo linaweza likasaidia sana. Hivyo hivyo na nyimbo tulizokuwa tunaimba za ukombozi wa Kusini mwa Afrika zilituhamasisha tukaona kwa kweli Tanzania haiwezi ikawa huru kabla ya Mataifa mengine haya kuwa huru; hatuwezi tukasema tuna uhuru kamili kama *South Africa* bado haijawa huru. Kwa hiyo, hiki ni kitu ambacho ninaamini tutaendelea kukifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana nilikuwa nasema tuungeze pia na elimu ambayo siyo *technical issues*; hii dhana ya kuteua mabalozi ilikuwa ni kuweka watu wa kuhamasisha waongee lugha ambazo wanaweza wakaongea kwenye masuala mengine ili waweweza kuelewana vizuri. Kwa hiyo, hii kwa kuwa na wenzetu wa Wizara ya Elimu wanaendelea kurejea rejea mitaala, naamini tutaendelea kuangalia. Mbona somo la Uraia liliweza kueleweka vizuri kwenye mambo ya *Multipartism*, ninaamini hata hilo litaendelea kueleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo imetolewa na imetolewa kwa uzito ambayo napenda nianze nayo, tumechangana sana hizi fedha za *TARURA* na katika maelezo, tulisema zinakwenda kwenye mfuko. Mfuko wa Maji uko moja kwa moja unatambulika na chanzo kile kitatoka kitakwenda moja kwa moja kwenye Mfuko wa Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye *TARURA* tumepokea maoni ya Waheshimiwa Wabunge na

wameelezea kwa kirefu sana kuhusu *set up* ya mfuko huu. Ndugu yangu Mheshimiwa Tabasam, ndugu yangu Mheshimiwa Kandege, Ndugu yangu Mheshimiwa Kakunda, ndugu yangu Mheshimiwa Kasalali Mbunge wa Sumve na nilimsikia Mheshimiwa Kyombo na Mheshimiwa Mwijage na Wabunge wengine wengi. Kama nilivyosema ni ngumu tu kutaja kila mmoja; lakini mlioliongelea jambo hili, tumelipokea na sisi tulivyokaa tukatafakari tukaona ni kweli muundo ule wa mwanzo ulikuwa unatumika kwa sababu kwa kweli *TARURA* ilikuwa inapewa *lift*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha ile llianza kama ya Mfuko wa Barabara lakini badaye tulivyooona huku nako kuna tatizo tukasema hawa wapate *lift*, lakini mapendekezo yanayosema sasa kama tumeweza kubaini chanzo kikubwa kinachotakiwa kwenda kwenye *TARURA*, *TARURA* sasa haipaswi kuendelea kuonekana inapewa *lift*, ilhali ina barabara nydingi kwa urefu inazotakiwa kuzihudumia. Kwa hiyo, tumekubaliana na pendekoz hilo la kuanzisha mfuko rasmi wa *TARURA* na wataalam wangu walishike vizuri, wafanye haraka maboresho hayo tutengeneze Mfuko wa *TARURA*.

Vyanzo vyake Waheshimiwa Wabunge mridhie wataalam wetu waviweke vizuri, ni shilingi 100 ambayo tumeipitisha hapa na asilimia 30 ile iliyokuwa inatoka kwenye mgawanyo ule uliopita; na vyanzo vingine ambavyo vilikuwa vimebainishwa awali kama vyanzo vya Mfuko wa *TARURA* viweze kuelekea pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwepo na matatizo madogo ya hapa na pale, nakumbuka kwa mfano kuna kipindi kimoja fedha ambayo ilitakiwa ipelekwe *TARURA* Agosti na Septemba ilikawia mpaka ikaja ikapelekwa mwezi Februari. Kwa hiyo, hoja za Wabunge walizotoa zina mashiko, nasi kama Wizara hatuwezi tukang'ang'ania jambo moja peke yake; hapa tunatengeneza mambo ya nchi, siyo mambo ya Wizara yetu, ni mambo ya nchi nzima na Waheshimiwa Wabunge mmekuja hapa kwa ajili ya kufanya jambo hili liweze kwenda vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naamini taratibu nyingine zitafuatia ambazo zitalifanya jambo hili liweze kukaa vizuri zaidi, lakini mantiki yake na uharaka ambao Mheshimiwa Rais anataka miradi iweze kutekelezwa, hatupaswi kuacha kitu chochote hapa kinachotuletea ukiritimba ambao unaweza ukatucheleweshea utekelezaji wa miradi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo Mheshimiwa Kunambi aliuliza kuhusu sheria ile tunaposema tutaweka utaratibu mwingine; akauliza utaratibu ule ni upi? Utaratibu ule, tuliosema tunataka kutengeneza Ofisi ya Msuluhihi wa masuala ya kikodi. Kwa hiyo, siyo utaratibu ambao utakuwa siyo rasmi. Tunataka tutengeneze Ofisi ya Msuluhihi wa Masuala ya Kikodi na huu ni utaratibu ambao upo *common*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nillivyoeleza siku ile ni kwamba itatutengenezea utaratibu kwa wale watu ambao wanataka tu masuala ya kueleweshana waende kwa mtu ambaye wanaweza wakaona kwamba kidogo ni *independent*. Ilivyokuwa sasa hivi ni kama tayari tulishatofautiana. Hata kama tungCAA tena sisi ambao tulishatofuatuana ni dhahiri kwamba kuelewana kwake kungeweza kuwa na ugumu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea maoni mengine likiwemo swalii la itakuwaje pale bei ya mafuta itakaposhuka? Tumelipokea jambo hili na kwenye Bunge hili Mheshimiwa Mwijage, Mheshimiwa Tabasam, Mheshimiwa Abood na Mheshimiwa Shabiby wametusaidia sana kwenye eneo hili la mafuta. Nami nawateua wawe washauri binafsi kabisa wa Waziri kwenye masuala haya ya uchumi wa gesi na mafuta; na Mheshimiwa Tabasam ongeza kabisa kwenye *CV* yako hii, kuwa wewe ni Mshauri wa Waziri wa Fedha kwa Masuala ya Uchumi wa Gesi na Mafuta. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona kwa sababu utaratibu unaotumika sasa hivi ni wa *bulk procurement* ambapo tunaagiza mafuta kwa wingi kwa ujumla, lakini pia kuna *administrative measures* ambazo zinafanyika na *EWURA*.

Tunaomba Wabunge waridhie hili jambo tulipokee kwanza, tulifanyie kazi ndani ya Serikali, halafu tuweze kuona kule mbele tunapokwenda. Tukiweka mabadiliko mengi kwa wakati mmoja na kwa wakati mfupi mfupi, *alignment* zake wakati wa utekelezaji inaweza ikatupatia shida kati kati yake. Waridhie, hii siyo bajeti ya mwisho, panapo uzima, Bunge litaendelea, tutakuja tena kushauriana yale ambayo tumeyapokea muda ukiwa umeshafika tuyafanyie kazi. Tujipe muda huu tuweze kuyarekebisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea hoja nyngi na nyngine tayari tulishaweka ile *budget framework*, tulishaweka mahesabu yetu na makadirio upande wa mapato na makadirio upande wa matumizi. Kwa maana hiyo, tukifumua tukaweka vyanzo vingine vya mapato na vikatuletea mapato mengi, tutakuwa tunalazimika turudi tena kule ambako utaratibu wetu wa kikanuni hata hauruhusu kwenda kufumua ambacho tulishapitisha kule. Kwa hiyo, nawaomba mridhie kwamba maoni mengine ni mazuri, tunayapokea, basi tutayafanya kazi kwa sababu tayari tulishapitisha bajeti kuu ambayo tumeshapitisha na *appropriation* yake ambayo inatulazimu mambo mengine yakae ndani ya vile ambavyo tayari tulishavipitisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo liliulizwa, ameuliza Mheshimiwa Maige pamoja na Wabunge wengine. Nimemsikia nadhani na Mheshimiwa Kunambi na wengine wengine wengi, naomba wananchi wenu waridhie tu kwamba ni ngumu kumtaja kila Mbunge, Iakini mmechangia hoja za msingi kabisa kwamba tutafanyaje fedha ya Luku kwa mtu ambaye angetaka kulipa mara moja? Vile vile tutafanyaje kwa sehemu ambayo mmiliki anataka kulipa yeeye mwenyewe?

Mheshimiwa Naibu Spika, jibu lake kama nilivyosema awali, jambo hili tunalifanya *programming*; kama ambavyo umeme huwa ukileta hitilafu, tunawaona wale wale *TANESCO*, umeme ukileta hitilafu nyumbani huwa tunawona, wapo mionganoni mwetu, huwa tunawaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiwa na jambo linahusu suala hili la utozaji wa *property tax* kwa njia hii ya Luku, ukaona kuja jambo unataka kulifanya, unawaona tu wana-*program* vile unavyotaka. Kwa maana hiyo, kama unataka iwe inalipwa mara moja, inakuwa *programed* kwamba inakatwa mara moja na haitakatwa tena. Kama unataka iwe *programed* mwanzo wa mwezi, itakuwa *programed*; kama unataka iwe *programed* kwa mgawanyo kufuatana na idadi ya hizo mita, hivyo ndivyo itakavyofanyika. Hivyo ndivyo teknolojia inavyorahisisha masuala ya utendaji wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo hivyo na kwa yule ambaye atataka aliye yeye mwenyewe, tumesema hawa watu hakuna mita ambayo haina mahusiano kabisa na mwenye nyumba, wala hakuna mita ambayo haitakuwa na uhusiano kabisa kabisa na wale waliopo, wala hakuna mita ambayo mtu atakuwa anaishi hana mahusiano kabisa. Hizi nyumba ni tofauti na vichuguu, wale wanaoishi mule anayetaka anaingia tu, kama kipo wazi unaingia. Hapa kuna *arrangement* nyingi tu. Kubwa ambalo kila mtu tumesema lazima alizingatie, ni kwamba hii ni sheria ya nchi. Hili ni jambo la kisheria. Kwa hiyo, maelezo yake hapo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kwa maghorofa yaliyo mengi, utaratibu wake ni ule ule; na tukawepa pia kwa wale ambao hawatakuwemo kwenye huu mfumo wataendelea kutumia utaratibu ule ambao ni *manual*/ambapo wataweza kukutana na wenzetu wa Serikali za Mitaa ambao tumewapa jukumu la *periodic* na *sport maintenance* ya barabara zetu ambapo tunaamini baadhi ya vyanzo vya mapato ambavyo wataendelea kuvipata wataongezea na hicho ili waweze kutekeleza utaratibu wetu wa kutengeneza hizo barabara kwa vipindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo lingine ambalo lilitolewa upande wa masuala ya boda boda. Maoni mapya aliyoyatoa Mheshimiwa Lugangila tunapokea na hiyo tutaongea na wenzetu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ambao ndiyo wenye sheria, kuangalia siyo tu kwa boda boda, ni kwa vyombo vyote vya moto. Hiyo ni *standard*

ambayo inaweza ikatumika kwa dereva ambaye amesharudia makosa ya aina ile ile kwa kipindi kirefu, hivi ataendelea kutozwa faini tu? Hyo tutaiangalia tuweze kuona utekelezaji wake hata huo utaratibu uliopendekezwa wa kutumia *points*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo nchi ambazo zinatumia utaratibu wa aina hii, lakini hili la kusema faini ikipingua kwamba kutoka shilingi 30,000/= mpaka shilingi 10,000/= kwamba vifo vitaongezeka, Waheshimiwa Wabunge kwa mtu ye yeyote akitusikiliza kwenye hiyo hoja, lazima aone, basi kama Taifa tutakuwa na shida kubwa sana. Tukiwa na Watanzania wanaogopa faini kuliko kifo, basi tuna tatizo moja kubwa sana la msingi, kwamba yeye kinachoweza kumfanya awe mwangalifu ni faini peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaposema ajali zinaua au uzembe unaua kwake yeye halilingii sana akili, kwamba yeye busara hiyo haionti, anaona faini ndiyo inaweza ikamfanya akaogopa sana faini ikiwa kubwa kuliko kifo, kuliko maisha ya wale waliowabeba, akaithamanisha sana shilingi 20,000/= ile kwamba ningelipa shilingi 20,000/= hawa ningewafikisha salama. Ningeongezewa na hii ikawa shilingi 30,000/= hawa ningewafikisha salama, kuliko thamani ya maisha yao wenyewe wale aliomwabeba, basi kutakuwa na tatizo kubwa sana la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyoamini, kwanza ukifanya tathmini ya wakati boda boda zinaanza kuingia hapa Tanzania na sasa, pana tofauti kubwa sana. Tunakwenda tunabadilika. Mwanzoni ilikuwa kawaida sana, huyu kijana asubuhi tu hapo anakabidhiwa boda boda kwa mara ya kwanza, anapiga *route* moja mpaka getini pale na kurudi, anabebe abiria. Sasa hivi wameendelea kutengeneza vikundi vyao na uongozi wao na wanaendelea kuelimishana wao wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu hawa boda boda wako majimboni kwetu, kila kijiwe tunao na wale viongozi wetu, hata sisi, hebu tutumieni

muda kuwaita hata wasiwe wote, tuwaite hata wale viongozi tu wa boda boda kwenye maeneo yetu. Tuwaite na tuwaambie neno moja tu kwamba jambo hili mnalofanya siyo la kibia shara pale yake, mnabeba uhai wa watu. Mnabeba maisha ya watu, lakini hata ninyi mnategemewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku moja tumewahi kwenda pale Jimboni kwangu kuongea na baadhi ya vijana humo, wakasema tunaelewana. Nimewahi kuzungukia na maeneo mengine, wakasema tunaelewana. Wakati mwininge zile *stress* na zenyewe za kukimbizana kwa ajili ya faini hizo na zenyewe zilikuwa zinasababisha ajali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi ninaamini, twendeni tuungeze elimu ya kusisitiza; wapite kwanza mafunzo kwamba awe ameshakuwa dereva anayeweza kuendesha, lakini pia mafunzo ya uungwana tu yale ya ustaarabu kuweza kuona kwamba amebeba maisha ya watu. Hili na lenyewe lipo ndani ya uwezo wetu na tunaweza tukafanya, tusiwaachie Polisi peke yake, hata sisi tunao uongozi kwao tuwaambie.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwaelezee hata wenzetu wa Tawala za Mikoa kule kwenye vikao vyao upande wa Madiwani kila Kata, ni eneo dogo tu. Diwani akitaka kuongea na vijiwe vyote vya boda boda anaweza akaongea nao, awaambie na wenyewe waendelee kukumbushiana; na viongozi wengine waliopo ngazi hizo waendelee kuwakumbushia. Hili ni jambo ambalo tunaweza tukalifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichokuwa kinasomeka, hakileti picha nzuri sana na ndiyo maana Mheshimiwa Rais aliona alisemee siku ile, kwamba hata tunapotoa makadirio ya mapato yetu, tunapotoa taarifa kwamba makusanyo yetu yalifanikiwa kwa kiwango gani, tunasema makosa yalipungua, kwa hiyo, hatukuweza kufikia lengo. Hii kiuchumi haileti taswira nzuri sana kuweka malengo kufuatana na makosa. Kwamba hawakukosa sana, kwa hiyo, hatukufikia malengo. Haisomeki vizuri sana hii. Pamoja na kwamba kifo kipo tu, ni sawasawa na biashara ya mtu alalamike kwamba

siku nzima leo majeneza yangu hayakutoka. Haileti picha nzuri sana kwamba kusema majeneza yangu hayakutoka, kwa hiyo, leo biashara yangu haikuwa nzuri kabisa. Kwa hiyo, hivi ni vitu ambavyo tunaweza tukavifanya kwa kutumia elimu na bado tukaweza kupiga hatua nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii haisomeki vizuri sana, ni sawasawa na biashara pamoja na kifo kipo tu, ni sawasawa na biashara ya mtu alalamike kwamba siku nzima leo majeneza yangu hayakutoka, haileti picha nzuri sana kwamba majeneza yangu hayakutoka, kwa hiyo leo biashara yangu haikuwa nzuri kabisa. Kwa hiyo hivi ni vitu ambavyo tunaweza tukavifanya kwa kutumia elimu na bado tukaweza kupiga hatua nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kanyasu ameongelea suala la nyasi bandia; niwaelekeze tu wataalam wangu kwa sababu Mikoa isiyo Manispaa ni mitano nadhani Simiyu, Geita, Njombe, Katavi na Manyara. Nadhani ni mikoa mitano ndiyo ambayo ni mikoa mipya ambayo imeongezeka ambayo si Manispaa. Wakati nasoma hapa nilisema tutaweka *provision* kwa ruhusa maalum kwa maeneo mengine ambayo yako tofauti. Kwa ushauri wa Mheshimiwa Kanyasu tutaongezea tu na Makao Makuu ya Mikoa ambayo haijawa Manispaa ili iweze kusomeka hivyo ili iweze kujumuisha na mikoa ile ambayo siyo manispaa wala siyo majji, lakini ilishafikia hatua ya kuwa mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni mengine tumeyapokea, kama hili alilolisema Mheshimiwa Kanyasu tumefanya kwa upande wa hospitali lakini bado kwenye shule, tunaomba mridhie na lenyewe tulipokee tuendelee kulifanya kazi zaidi kwa sababu kwa sasa tumeshaweka fremu yetu ya mapato na tunaamini kwamba haitakuwa vizuri sana tukifanya muda huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Tadayo aliongelea kuhusu *TRA* kuendelea na masuala ya elimu ya mlipakodi tumepokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kigwangala aliongelea habari ya kodi ya majengo nimeetoka kulifafanua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ali King pamoja na ndugu yangu ambaye ametoka kumalizia amesemea habari ya upande wa Zanzibar. Tulisema yale marekebisho tuliyoyafanya, yale marekebisho tumeyafanya, tena tumeyafanya kwa kushirikiana pande zote mbili. Nilikutana na Mheshimiwa Waziri wa Fedha wa Zanzibar akiwa na timu yake ya wataalam na mimi nikiwa na timu yangu ya wataalam, tukayarekebisha yale ambayo tuliyarekebisha na kwa mwaka huu tukakubaliana tuanzie hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtakumbuka tumeanza kazi tukiwa tayari Mabunge ya Bajeti yanaendelea kwa maana hiyo kazi ya kwanza ambayo imebidi tuje tuifanye ilikuwa ni ya kuandaa nyaraka hizi za bajeti. Tumepanga kuendelea kukutana kuangalia mengine ambayo bado yanaleta manung'uniko, baada ya bajeti tutaendelea kufanyia kazi mengine. Inakuja sheria hii ambayo ilikuwa inaleta usumbuwa vyombo moto kutoka upande mmoja kuja upande mwengine, tunalifanya kazi na tutakuja na jawabu la kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunaenda kwenye lile jambo kubwa zaidi la mambo ya Mfuko wa Pamoja, tunataka tujue kwanza *numbers* zinasemaje kwa sababu eneo moja la kuanzia nadhani ni pale kwenye *numbers*, zinasemaje kwenye yale mapendekezo ambayo mara zote yamekuwa yakiongelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu haya ya mapato ambayo pande zote ziko mbili; tunatumia sheria ile ile ambayo ipo, kwamba, kama ambavyo tunatumia kwenye *exercise* ya sasa hivi, kwamba fedha ambazo zinakatwa pale zilipotokea ndipo zinakotumika kama tulivyofanya kwenye masuala ya uhamiaji, pale zinapotokea ndipo zinapotumika. Hii ni rahisi tu, kama mtu anatuma *M-pesa* yuko Zanzibar na tukakata maana yake fedha ile iko pale pale. Kama aliyetoa yuko pale pale na tunakata fedha ya kutolea, maana yake

iko pale pale. Kwa maana hiyo na mitambo ambavyo inarahisisha maana yake lile halina tatizo kabisa, fedha zile ambazo zimetumwa ama kutolewa kwa upande wa Zanzibar zitatumika pale Zanzibar na zile ambazo zimetolewa Bara ama kutumwa Bara zitatumika Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, kwa heshima na itifaki ya mamlaka, kitu pekee ambacho hatuwezi tukafanya ni kuzipangia fedha zile ambazo zimepatikana kwa upande wa Zanzibar zitumike wapi, ile ni mamlaka na wenyewe watapangia ziweze kutumika wapi. Hili ni jambo ambalo tunaweza kulifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Waheshimiwa Wabunge, nina matarajio kwamba tunaenda kukusanya fedha, tutapata fedha. Naendelea tu kulisitiza hili jambo, ndiyo maana sikubishana sana na Waheshimiwa Wabunge wakati wanatoa maoni tuzitumieje hizi fedha, tuzilinde vipi hizi fedha na ndiyo maana niliona tutumie hayo mawazo kwa sababu fedha hizi ni za wananchi na uamuzi huu tumeufanya pamoja, kwa hiyo twendeni tukasimamie. Naamini tutakapokuwa tumefanya jambo hili, tutafungua uchumi na kadri tunavyofungua uchumi kwa kufungua barabara, kwa kufungua masuala ya huduma zingine za jamii, naamini uchumi wetu utaendelea kupanda na tukishatoka hapo tuaenda kuyafanya kazi mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mawili ya mwisho kama utaridhia dakika mbili zako, jambo la kwanza ni hili ambalo lilijitokeza la upande wa hii *transfer mispricing*, ambayo tulikuwa tunaiiongelea hii *transfer pricing*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitoka kwa ajili ya kuwahi kuja kupokea hoja hapa, lakini Kamati pamoja na wajumbe waliokuwepo kule, makubaliano waliyofikia ni kufanya mabadiliko. Kwenye pendekozu tulilokuwa tunapendekeza kuweka asilimia 75, wanapendekeza iwe asilimia 100 ya kodi iliyo takiwa kutozwa. Kwa maana hiyo kodi itakuwa imezidishwa mara mbili ya ile ambayo ilitakiwa itozwe kama huyo mta hakuikwepa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Serikali kama nilivyosema, tunapokea maoni ya Waheshimiwa Wabunge na Kamati ni mwakilishi wa Bunge, wamependekeza hilo pendekezo. Kwa hiyo hicho ndicho ambacho wataalam wangu watakiandika kama Kamati ya Bunge ilivyopendekeza, marekebisho hayo yaingie kama yalivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo moja la mwisho, imeongeleta hii habari ya *Withholding* kwenye kilimo na naomba na Waheshimiwa Wabunge tusikilizane vizuri sana kwenye jambo hili. Hiki ambacho tumekipendekeza hakiendi AMCOS wala hakiende kwa mkulima mdogo na *withholding nature* yake jinsi ilivyo, yule ambaye anatozwa hii kodi, huyu mtu wa kati anayeshughulika kwenye hiyo biashara, mwisho wa siku anai-recoverile fedha kama hakustahili kuilipa kupitia yale mapato yake, ana-offset, atakuwa tu ni yule ambaye atakuwa bahati mbaya sana akitaka kuipasisha iende kwa mkulima. Kwa sababu hii hapa ina kuwa sehemu wakati ana *calculate* yeye kodi zake za mwaka, inakuwepo, ndiyo *nature* ya *withholding tax* zinavyofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiki kitu tulichopendekeza *NFRA* na Bodi ya Mazao Mchanganyiko wana *withholding* hiyo ya 2% hiyo hiyo. Tulisema kama hawa wanafanya biashara eneo lile lile na soko lile lile, kwa nini *NFRA* wanafanya na Bodi ya Mazao Mchanganyiko wanafanya na hawajawahi kuathiri wakulima wetu na hata wakulima wote huwa wanapenda mazao yao wauze *NFRA*, tuliona tunaweza tukawianisha ili tuweze kuendelea nalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni yangu ni vile muda huu ulikuwa mfupi sana, nikiri kwamba hatukufanya mengi zaidi kwenye sekta hii ya kilimo tumekaa na wenzetu wa Kilimo pamoja na Mifugo, tukasema kwa kuanzia tuanze na bajeti zilizokuwepo, lakini pia tuanze na maeneo tunayoweza kuchochea masuala haya ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, safari tuliyonayo kwenye Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ni ndefu sana. Ni

safari moja ndefu sana na siku tuki-*mechanize production* kwenye kilimo mifugo na uvuvi nchi yetu hii uchumi wake ukanda huu wa Afrika labda tutakuwa tunapambana na South Afrika sijui na nani mwengine, kuna kazi kubwa sana tunatakiwa kufanya. Kazi hii lazima tufanye tathmini ya *measures* tunazofanya kwenye kilimo, mifugo na uvuvi, zimesaidia kwa kiwango gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, angalia tangu tuanze kukata hizi tozo, tufanye *comparison* tujuje kwanza tozo hizi ambazo tumewahi kuziondoa hivi zina *amount* kiasi gani na je, zimesaidia kwa kiwango gani? Nilimsikia Mheshimiwa Spika siku moja akiwa amekaa pale nadhani siku ya Bajeti ya Kilimo, akawa anajiuliza tu swalí fikirishi, hivi hii bajeti hata kama ingeenda yote hivi ingemfikiaje mkulima, alikuwa anajiuliza hivyo. Swalí linabaki pale pale hizi *measures* tunazofanya kwenye hili Sekta kubwa hili za Kilimo, Mifugo na Uvuvi hivi ni kweli zime-*transform* hizo sekta?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukirudi ukaangalia ni nini kinachotakiwa jibu linakuja siyo. Moja, ili kilimo chetu tuki-*transform* na tunakaa sana vikao vingi na Wizara ya Kilimo, Mwalimu wangu Prof. Mkenda pamoja na Mheshimiwa Bashe, tunawaza tukibadilishie wapi hiki kilimo. Maeneo ambayo tunatakiwa tuguse ili kiweze kubadilika kilimo, mifugo na uvuvi kwa kiwango kikubwa bado tunahangaikia huku kwenye *administrative issues*, kwa maana hiyo panakazi kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe Waheshimiwa Wabunge waridhie, kwa sasa hivi na kwa muda tulionao tuendelee kwa sababu tumesha-*fix tax measures* zetu pamoja na makadirio, lakini waturuhusu sisi tunesema tukimaliza tu hivi tunaanza kujandaa kuhusu hizi sekta. Siku tuki-*transform*, sasa hivi nikiwa namalizia tu neno la mwisho, ukienda kule vijijini kazi hii ya kilimo inafanywa tu na wazazi wetu na babu zetu, hiki kizazi cha leo hakifanyi kwa sababu uzalishaji unaotumika ni wa zamani. *Graduates* wengi hawawezi wakafanya shughuli ya uzalishaji uliokuwa unafanywa na bibi zetu, wanahitaji tutengeneze

mechanization ambayo watazalisha kisasa na watakopesheka kwenye mabenki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tuna kazi kubwa sana. Wabunge waridhie, tutakuja na mapendekezo huku tuki-*implement* kidogo kidogo haya ambayo tumeshaongea na wenzetu wa Wizara ya Kilimo pamoja na ile ya Mifugo na Uvubi, kuna kazi kubwa sana tunatakiwa kufanya hapa. Tunaongea hata na Wizara ya Maji kwamba kuanzia sasa miradi mikubwa watakayo-*design* kama ni mradi wa kutoka Ruvuma kwenda baharini yaani miradi yote ya kwenye mito mikubwa inayomwaga maji baharini waki-*design* mradi mkubwa wa maji kwa matumizi ya nyumbani waweke na matoleo kwa ajili ya maji ya umwagiliaji, ili siku tukitaka kutengeneza umwagiliaji tusihitaji kulaza bomba lingine. Tuna kazi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu ambao wananchi kame wanamwagilia, lakini sisi bado tunahangaika na zile *administrative*. Ukiangalia hatua zilizokuwa zinatumika, kuna wakati tulikuwa tunasema watu wakikosa chakula tunawapelekea chakula cha msaada, hii haikuwa *sustainable*. Kuna muda tukasema watu wakikosa chakula hatutawapa, hii na yenye siyo *sustainable*, iliyio *sustainable*, kama wakilima mara moja wanakosa chakula tuwafanye walime mara mbili na wavune mara mbili ili waweze kupata kile chakula. Kwa hiyo haya ndiyo mambo ambayo tunataka tuangalie tunaweza tukayafikia kwa namna gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabisa, niwatakie kila la kheri Mheshimiwa Mwakasaka, Mheshimiwa Bashe na Mheshimiwa Gulamali, tuna jambo letu kule Tabora. Hebu waende wakafanye kazi ile ya ukombozi ambayo iliyahi kufanywa na Chama Cha Mapinduzi na TANU pamoja na timu ya Yanga ambao walishiriki kuikomboa Tanzania pamoja na Nchi za Kusini mwa Afrika. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwa nimeyasema hayo, naomba sasa kutoa hoja ili shughuli zingine ziweze kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.
(Makofii)

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono, tutaendelea na utaratibu wetu. Katibu.

NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI: Kamati ya Bunge Zima.

NAIBU SPIKA: Kamati ya Bunge Zima.

KAMATI YA BUNGE ZIMA

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

Kifungu cha 1

Kifungu cha 2

Kifungu cha 3

Kifungu cha 4

Kifungu cha 5

Kifungu cha 6

Kifungu cha 7

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 8

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Kifungu cha 9

Kifungu cha 10

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 11

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 12

Kifungu cha 13

Kifungu cha 14

Kifungu cha 15

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 16

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 17

*(Kifungu kiliviyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 18

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 19

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu Kimepitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 20

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu 21

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilifutwa na Serikali)

Kifungu cha 22

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 23

*(Kifungu kiliviyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 24

(Kifungu kilichotajwa hapo kilifutwa na Serikali)

Kifungu 25

Kifungu 26

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 27

Kifungu cha 28

Kifungu cha 29

Kifungu cha 30

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 31

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilifutwa na Serikali)

Sehemu ya Kumi

Kifungu cha 32

Kifungu cha 33

Kifungu cha 34

(Sehemu ya Kumi ya Muswada ilifutwa na Serikali)

NAIBU SPIKA: Sasa hapa nilitarajia kwamba baada ya kufuta hivi vifungu kuwe na marekebisho ya hizi namba.

Waheshimiwa Wabunge, nimeoneshwa hapa katika marekebisho ya Serikali yaliyoletwa kuna sehemu ambayo wanapendekeza kufanya marejeo ya hizi namba ili zibadilike na pia hizi sehemu. Kwa hiyo tutazihoji zote kwa pamoja wakati huo.

Kifungu cha 35

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

NAIBU SPIKA: Sasa Katibu hiki kifungu kikihojiwa kama cha 35 kitakuwa kifungu namba ngapi. Kwa utaratibu wetu ilibidi hizi namba zisomwe mpya ili Wabunge wajue wanahojiwa namba gani, lakini sasa kwa sababu hawajatayarisha na huo ndiyo utaratibu, ilibidi hapa ziwe zimeandikwa zile namba na sehemu ziwe zimebadilika kulingana na haya marekebisho yaliyoletwa na Serikali. Ndiyo utaratibu kwa sababu tukihojiwa 35 halafu 35 itakuja kuwa ni namba tofauti ikija kubadilishwa.

Kwa utaratibu wetu ilibidi hizi namba ziwe zinasomwa kwa namba mpya baada ya wao kuwa wameweka.

Haya tuendelee, Katibu.

Kifungu cha 36

Kifungu cha 37

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 38

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Kifungu cha 39

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 40

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 41

*(Kifungu kilivyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 42

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 43

*(Kifungu kilivyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 44

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 45

Kifungu cha 46

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 47

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 48

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 49

Kifungu cha 50

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI: Sehemu ya 18 ya Muswada inapendekezwa kufutwa ambayo ni vifungu vya 51 na 52.

Sehemu ya Kumi na Nane

Kifungu cha 51

Kifungu cha 52

(Sehemu ya Kumi na Nane ya Muswada ilifutwa na Kamati ya Bunge Zima)

Kifungu cha 53

(Kifungu kiliviyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 54

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Kifungu cha 55

(Kifungu kiliviyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 56

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Kifungu cha 57

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *part (xxi)* naomba unisaidie kuanzia kifungu cha 57 mpaka kifungu cha 73 Waziri alikuwa alete *amendment* aidha ya *Section 55 or Section 59* ku-reflect ile adhabu wanayotaka kuitoa kwenye *transfer price regulation* kuileta kwenye adhabu ya *Tax Administration Act*.

MWENYEKITI: Sasa kwa sababu umesema ni sehemu hii, na umetaja vifungu mahususi, viro vifungu vinaongezwa huku mbele; sijui kama hayo marekebisho na wewe unayo ama huna.

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nililetewa marekebisho yakawa *withdrawn* sasa sijui kama bado yapo mezani. Nililetewa *further schedule* lakini na yenye ikawa *withdrawn* kwa hiyo, nilikuwa nataka njue kama *further schedule* ipo mezani naomba nakala.

MWENYEKITI: Zipo nyingi nyingi hapa, ngoja tuangalie hicho kifungu ulichokitaja japokuwa hatujakifikia. Kinaongezwa kifungu namba 71, unayo hayo marekebisho ama hauna?

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sina.

MWENYEKITI: Nadhani tutakapofika hapo utakuwa umeshasoma na kupitia.

(Kifungu kilivyatjwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 58

Kifungu cha 59

Kifungu cha 60

Kifungu cha 61

Kifungu cha 62
Kifungu cha 63
Kifungu cha 64
Kifungu cha 65
Kifungu cha 66
Kifungu cha 67

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 68

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Kifungu cha 69
Kifungu cha 70

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu Kipyä cha 71

MWENYEKITI: Serikali inapendekeza kuongeza kifungu kipyä cha 71 kwa maelezo aliyo kuwa ameyatoa Mheshimiwa Waziri hapa wakati akihitimisha hoja yake na kifungu hicho tunacho hapa mbele ambacho kinasema ni nini kitabadi lishwa.

Kwa hiyo, alivyosema kwamba ile adhabu itakuwa asilimia 100 na hapa ndicho kilicho andikwa.

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 71 kinachopendekezwa kuongezwa cha ku-amend section 79 ya *Tax Administration Act* kina nia ya kutekeleza hoja ya Mheshimiwa Waziri ya kufuta ile adhabu ya 100 percent ya *transfer pricing transaction* na kui-replace na asilimia 100 ya kodi itakayokokotolewa baada ya mtu kubainika kwenye ukaguzi ame-transact on *transfer mispricing*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Kamati yako itambue madhara ya kifungu hiki haiendi kurejesha kile kilichotolewa, inaenda kupunguza adhabu kwa hizi *multinationals* kwenye maeneo ya *transfer mispricing* ambayo ni maeneo sugu sana kwa ukwepaji wa kodi kwa makampuni ya Kimatifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwenye eneo hili nisilunge mkono, nipendekeze kifungu hiki kiondolewe na Kibaki kile kifungu cha *transfer pricing regulation*.

MWENYEKITI: Sasa Waheshimiwa Wabunge kwa kawaida mabadiliko yakiletwa ili mabadiliko ya Mheshimiwa Mbunge yaingie humu lazima na yeye awe ameleta mabadiliko yake. Sasa kwa sababu ya jambo lenyewe namna liliyvo, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kwa sababu ndio mlikuwa na kikao huko. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Makamu Mwenyekiti hebu elezea kidogo hili jambo. (Makof)

MHE. OMARI M. KIGUA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi ni kwamba tulikutana asubuhi na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na timu yake yote halikadhalika na Wajumbe wa Kamati ya Bajeti lakini pia tuliwaalika Waheshimiwa Wajumbe mbalimbali akiwemo Mheshimiwa Silaa. Baada ya maelezo ya kutosha kabisa, mabadiliko ambayo yameletwa mbele ya meza yako ndio ambayo tumekubaliana yote kwa pamoja kwamba ndio msimamo wa Bunge lako. (Makof)

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Mwenyekiti,...

MWENYEKITI: Eh! Subiri kwamba Mheshimiwa Jerry, hebu wataalam huku nyuma mnayo ile *Principal Act*, mnayo hapo? Waheshimiwa Wabunge ngoja nипитие kile kifungu kwenye sheria mama.

Waheshimiwa Wabunge nadhani mawanzoni marekebisho yaliyokuwa yameletwa ni kwamba kuwe na

asilimia 75, hii ndio yenyewe marekebisheso au ni kabla ya marekebisheso? Kabla ya marekebisheso ya Waziri, sawa!

Sasa kama ni kabla ya marekebisheso ya Waziri, kinachoongezeka hapa pengine kwa namna mimi nilivyokisoma hapa mbele, nikubaliane na maelezo ya Mheshimiwa Kigua ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa sababu nimeitisha ile sheria mama yenyewe, nimeipitia hapa na haya marekebisheso yanayoletwa naona hapa kuna hiyo *for a person who has contravened subsection 1(c) ambayo (c) ipo hapa hiyo mpya ndio wanaesema one hundred percent of the tax short form.* Maana yake ile kodi ambayo ameikwepa ndio ambayo wanaenda kumpa adhabu; ndivyo kifungu kinavyosema hapa. Na amekwepa mazingira gani imeelezwa sasa kwenye hii (c) ambayo ipo hapa. (*Makofi*)

Kwa hiyo, nadhani Mheshimiwa Mwenyekiti kwa sababu Kamati ilikubaliana na haya marekebisheso, twende nayo kwa namna hiyo. (*Makofi*)

*(Kifungu Kipywa cha 71 kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima
bila mabadiliko yoyote)*

MHE. JERRY W. SILAA: Mwenyekiti,...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jerry.

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niiambie tu Kamati yako ya Bunge hili kwamba sisi tulialikwa kwenye Kamati ya Bajeti tukatoa maoni yetu lakini hatukushiriki kwenye maazimio ya kikao. Kwa hiyo, hilo kwanza liwekwe kwenye kumbukumbu sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili; kifungu cha 79 kinachoenda kurekebisheswa tayari ni kifungu kipo kwenye *Tax Administration Act* ambacho kinatoa adhabu kwa watu wanaokwepa kodi. Kinachofanyika sasa hiki kinachoongezwa kinaenda kufuta Kanuni maalum ya *Transfer Pricing* ambayo ni mfumo tofauti kabisa wa ukwepaji wa kodi

wa multinationals na kurudisha kifungu kile kuja kwenye Sheria hii mama kuja kuwa *treated* kwenye hiyo section 79 kifungu kinachoongezwa cha (c). Na msimamo wangu ulikuwa ni kutokuwa na kifungu hiki kwenye mabadiliko ya 71 na kubaki na ile *Transfer Pricing Regulation* ambayo inatoza asilimia 100 ya *transaction* itayobainika upon audit ya kuweza kufanya *transfer pricing*.

MWENYEKITI: Sawa, sasa Waheshimiwa Wabunge nimemruhusu Mheshimiwa Jerry Silaa azungumze kwa sababu tupo katika kujifunza. Kwa utaratibu wa Kikakuni, ni kwamba ili upate fursa ya kuzungumza kwenye kifungu lazima uwe umeleta hapa mbele andiko lako, ndio Kanuni zetu zinavyotaka lakini nimempa fursa, huu sio utaratibu wa kawaida. Kwa hiyo, kule mbele mtakuwa mnashangaa tu kifungu kinahojiva halafu tunasonga mbele. (*Makofii*)

Lakini utaratibu aliousema ndio upo Kikanuni hasa, Kamati inaruhusiwa kualika watu amba wanataka kushiriki kwenye mjadala wa hoja fulani. Wakati Kamati inafanya maamuzi, hao wageni si sehemu ya yale maamuzi. Ni utaratibu wa Kikanuni kabisa. (*Makofii*)

Naona Mheshimiwa Waziri umefungua hapo, unataka kutoa maelezo ya ziada ama? Kwa sababu kifungu hata hivyo kimeshahojiwa Mheshimiwa Waziri yaani nilimpa tu nafasi azungumze lakini kifungu kimeshahojiwa na Bunge limeshaamua. Kwa hiyo, kifungu kiko namna ambavyo... (*Makofii*)

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kuweka kumbukumbu sahihi kama utaniruhusu. Nilishapeleka mapendekezo ya *schedule of amendment* na nilikuwa nasubiri hii *further schedule of amendment* ambayo umenikabidhi wewe hapa ndani ya ukumbi. Nilikuwa nangoja nikikabidhiwa hii, na mimi nikabidhi ya kwangu mezani...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jerry, sasa kwa utaratibu ulivyo, ukipeleka haikuja hapa mbele yaani sio suala la Bunge kuiitisha hiyo ije; kama haikuja hapa ni kwamba haijafika na

sijaiona. Na kwa hivyo, huwa siitazami kwa sababu sina cha kutazama, moja.

La pili, hata kama hoja yako ingekuwepo hapa mezani, utaratibu wa maamuzi ya Bunge ni kuhojiwa. Kwa hiyo, ungeleta hiyo hoja yako, Bunge lingefanya maamuzi, linataka wazo lako au linataka wazo la Waziri, ndio utaratibu wake. Kwa hiyo, haimaanishi kwamba ya kwako ingekuwa hapa lazima Bunge lingekubaliana na wewe.

Kwa hiyo, hata hapa bado Bunge lingehojiwa na lingefanya maamuzi. Kwa hiyo, sio lazima wazo lako ndio lingepita humu ndani. Sasa kwa sababu sina hicho unachosema wewe ulileta ukawa unasubiri ya Waziri, basi ya Waziri ndio niko nayo hapa mbele na Bunge limeshafanya maamuzi kuhusu kifungu hicho. (*Makofi*)

Katibu tunaendelea.

Kifungu cha 72
Kifungu cha 73
Kifungu cha 74
Kifungu cha 75
Kifungu cha 76
Kifungu cha 77
Kifungu cha 78

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 79

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Kifungu cha 80
Kifungu cha 81
Kifungu cha 82

Kifungu cha 83

Kifungu cha 84

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 85

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 86

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 87

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 88

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na marekebisho yaliyofanywa na Serikali, Muswada wa awali ulikuwa na Sehemu 25 sasa inapendekezwa Muswada huu uwe na Sehemu 23.

*(Sehemu Ishirini na Tatu za Muswada yalipitishwa na
Kamati ya Bunge Zima)*

NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na marekebisho ya Serikali Muswada wa awali ulikuwa na vifungu 88 sasa kwa mabadiliko yaliyofanyika Muswada utakuwa na vifungu 84.

*(Vifungu themanini na nne vya Muswada vilipitishwa na
Kamati ya Bunge Zima)*

NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imemaliza kazi yake.

MWENYEKITI: Bunge linarejea!

(Bunge Lilirudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Tukae, mtoa hoja taarifa.
(Makofi)

TAARIFA

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2021 (*The Finance Act, 2021*), kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake. Naomba kutoa hoja kwamba taarifa sasa ikubaliwe rasmi na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.
(Makofi)

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Sasa kwa utaratibu wetu nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja illamuliwa na Kuafikiwa)*

NAIBU SPIKA: Hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango imepita na sasa nimuite Katibu kwa hatua inayofuata. Katibu.

NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI: Muswada wa Sheria kwa ajili ya kutunga sheria itakayotoza au kubadilisha baadhi ya kodi, ushuru, tozo na ada mbalimbali, kufanya marekebisho kwenye sheria mbalimbali zinazohusu ukusanyaji

na usimamizi wa mapato ya umma (*A Bill for an Act to impose and alter certain taxes, duties, levies, fees and to amend certain laws relating to the collection and management of public revenues*).

(Kusomwa mara ya Tatu)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kwa taratibu zetu za Kikauni lakini pia taratibu zetu Kikatiba, sasa Bunge limemaliza kazi yake kwa maana ya kutunga sheria na sasa Muswada huo umeshapitishwa na Bunge. Na kwa mujibu wa Katiba yetu Ibara ya 97, utapelekwa kwa Mheshimiwa Rais ili upate idhini yake na uwe sasa sheria. Kwa hiyo, atakapotoa kibali hicho Mheshimiwa Spika atapata taarifa kwamba sasa hii imekuwa sheria.

Nichukue nafasi hii kutangaza kwamba sasa Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2021 (*The Finance Bill, 2021*) umepitishwa na Bunge. (*Makofii*)

Kwa muktadha huo huo nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wataalam wote wanaofanya kazi chini yenu kwa kazi nzuri mliyoifanya juu ya hii Sheria lakini pia namna ambavyo mmekuwa na ushirikiano wa karibu sana na Kamati yetu ya Bajeti na kusikiliza mawazo yao ambao wanafanya kazi kwa niaba yetu sisi wote lakini pia mawazo mbalimbali ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wabunge hapa wakati wakichangia Muswada huu.

Waheshimiwa Wabunge, yote mmeyasikia na Mheshimiwa Waziri umesema hapa wakati ukihitimisha yako mambo ambayo pengine tungekuwa hatujafika mwisho kwa maana ya Bunge hili kwamba limeshaamua ni kiasi gani cha fedha imeidhinisha, pengine kungekuwa na mabadiliko ya hapa na pale maana yake ni kwamba Waheshimiwa Wabunge michango yote ya mawazo mnayoitoa ya mawazo Serikali inaichukulia kwa uzito kabisa ninyi kama wawakilishi wa wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Waziri ameeleza hapa kwamba wataendelea kuyachakata hayo mawazo yenu ili baadae waweze kuyafanya kazi kwa sababu hiki tulichokifanya kipindi hiki ni bajeti ya mwaka mmoja, na mwakani kipindi kama hiki tutakuwa tukifanya haya tunayoyafanya sasa. Na ni Dhahiri mawazo yenu Waheshimiwa Wabunge mengi yatakuwa yameingia huko kwenye michakato ambayo wenzetu wanapotuletea mpango, basi tutaanza kuyaona mawazo yetu huko.

Kwa hiyo, niwapongeze upande wa Serikali kwa kusikiliza mawazo ya wananchi ambayo yanapita kwa Waheshimiwa Wabunge. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, shughuli zilizokuwa zimepangwa kwa ajili kufanywa leo zimekamilika na kwa hilyo naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3 kamili asubuhi. (*Makofii*)

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Ijumaa,
Tarehe 25 Juni, 2021 Saa Tatu Asubuhi)*